# Nipashe

Ijumaa Juni 19, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580262

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN




## Baba adaiwa kubaka watoto wake 3, mmoja apata ujauzito

UKURASA 8

## BAA LA CORONA



Kumbuka kupata taarifa za Covid-19 kupitia Shirika la Afya Duniani (WHO) na mamlaka zinazohusika nchini kutoa taarifa hizo kama Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ili kujilinda na maambukizi ya ugonjwa huo.

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## MLOGANZILA YATIBU MAWE KWENYE FIGO BILA UPASUAJI

UKURASA 8

# Mchuano mkali urais wa Z'bar

- Tisa wachukua fomu kumrithi Shein, yumo Shamsi Nahodha ... *Endelea Uk. 2*












Waziri Kiongozi mstaafu, Shamsi Vuai Nahodha (kulia), akichukua fomu ya kuomba uteuzi kugombea urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika Ofisi Kuu ya CCM, Kisiwandui, mjini Zanzibar jana. Wengine waliochukua fomu ni Muhamed Jafar Jumanne (juu kushoto), Balozi Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor (chini kushoto) na Mohammed Hija Mohammed (juu kulia). **PICHA: RAHMA SULEIMAN**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Ratiba ya uchaguzi mkuu ndani ya siku 5

UK. 2

**MICHEZO** JKT YALALAMIKA YANGA KUBEBWA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Mchuano mkali urais wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UNAWEZA kusema ni mchuano mkali katika mbio za kuwania uteuzi katika Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya kugombea urais wa Zanzibar uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Makada zaidi wa chama hicho wanaendelea kujitokeza kuchukua fomu, ambapo jana wanne walichukua fomu hizo.

Kujitokeza kwa makada hao kumeongeza idadi ya waliochukuwa fomu kufikia tisa, baada ya Jumatatu kujitokeza makada wawili na Jumatano kujitokeza watatu.

Waliojitokeza jana ni Waziri Kiongozi mstaafu, Shamsi Vuai Nahodha, Mohamed Jaffar Jumanne, Muhammed Hija na Balozi Meja Jenerali mstaafu Issa Suleim Nassor.

**SHAMSI VUAI NAHODHA**

Nahodha alitangulia kufika katika Ofisi ya CCM Kisiwandui majira ya saa mbili asubuhi na kukabidhiwa fomu hiyo na Katibu wa Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) CCM Zanzibar, Galous Nyimbo, huku akipewa fomu tatu zikiwamo za kutafuta wadhamini katika mikoa mitano ya Zanzibar ikiwamo mmoja wa Pemba.

''Karibu Mheshimiwa, nakukabidhi fomu hizi tatu ikiwamo ya kutafuta wadhamini wapatao 250 katika mikoa mitano ya Zanzibar ikiwamo mmoja wa Pemba na kuzirudisha kwa kuzijaza ifikapo Juni 30," alisema Nyimbo.

Nahodha alizipokea fomu hizo na kutoa Sh. milioni moja zikiwa fedha za ada kwa ajili ya fomu.

''Ndugu zangu na marafiki zangu waandishi wa habari leo sitozungumza na waandishi wa habari...wekeni maswali yenu yawe magumu tutapanga siku nyingine nitakuwa tayari kuzungumza na nyingi," alisema.

Hii ni mara ya pili kwa Nahodha kuchukuwa fomu ya kuwania urais wa Zanzibar, kwani katika mwaka 2000 wakati huo akiwa Waziri Kiongozi, alichukua fomu na kushindana na Rais wa sasa, Dk. Ali Mohamed Shein wakati huo akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na kutopitishwa na vikao vya juu vya CCM.

**MOHAMED JAFFARI JUMANNE**

Majira ya saa tano asubuhi, Mohamed Jaffari Jumanne alichukua fomu huku akikataa kuzungumza na waandishi wa habari kwa madai kwamba hajajitayarisha.

''Waandishi wa habari nimechukua fomu ya urais wa Zanzibar na sasa nipo katika harakati za kutafuta wadhamini 250, lakini sipo tayari kuzungumza na waandishi wa habari kwa sababu sijajiandaa," alisema.

Aidha, majira ya saa 7:30, kada mwingine, Muhammed Hijja, alifika katika Ofisi za CCM, lakini na yeye pia hakuzungumza na waandishi wa habari.

Hijja aliwahi kuwa Ofisa Mwandamizi katika ubalozi wa Tanzania nchini India na pia alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa kwa upande wa Zanzibar katika miaka ya 1990-2000.

''Nimekabidhiwa fomu za kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar na kazi yangu ya kwanza ni kuzipitia na kutafuta wadhamini...kwa hivyo naomba nipeni muda zaidi," alisema.

**BALOZI MEJA JENERALI ISSA SULEIMAN NAASOR**

Balozi Meja Jenerali, Issa Suleiman Naasor, alifunga zoezi hilo kwa siku ya jana, ambaye alikuwa wa mwisho kuchukua fomu hiyo aliyefika majira ya Saa 7:46 mchana.

Kada huyo wa CCM ni mwanadiplomasia na aliyewahi kuwa balozi wa Tanzania nchini Misri.

Meja Jenerali Nassor akizungumza na waandishi wa habari, alisema anataka kuimarisha umoja, mshikamano na uzalendo, huku kila mtu akiwa na nafasi ya kufanya kazi na kutoa mchango kwa maendeleo katika nchi yake.

Alisema utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM itakuwa ndiyo mwongozo na dira katika kuongoza nchi na kuleta maendeleo ikiwamo kukuza uchumi.

''Nitasisitiza na kuhimiza uzalendo... tuwe na uzalendo wa kupenda nchi yako, utaifanyia nini Zanzibar na sio wewe ikufanyie nini nchi yako," alisema na kuongeza: "Nataka kuwaunganishe watu wote bila ya kujali itikadi zao za kisiasa," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri (wa pili kulia), akipokea Sh. milioni 34.5 kutoka kwa Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wa Mkoa huo, Mussa Chaulo, kwa ajili ya kuwakabidhi viongozi wa CWT SACCOS Manispaa ya Tabora, baada ya kuokolewa na taasisi hiyo, kutokana na baadhi ya viongozi wa bodi ya zamani ya SACCOS hiyo, kujikopesha na kushindwa kuzirejesha. **PICHA: TIGANYA VENCENT**.

## NEC kutangaza rasmi tarehe ya uchaguzi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi nchini (NEC), imesema tarehe rasmi ya uchaguzi mkuu, mwaka huu, itatangazwa baada ya kutolewa kwa tangazo kwenye gazeti la serikali la kuvunjwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Wapigakura, Mkurugenzi Mtendaji wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema tarehe rasmi ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwaka huu, itatajwa baada ya kuona tangazo kwenye gazeti la serikali.

"Rais Magufuli alivunja Bunge ili kutangaza tarehe rasmi ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu, tunasubiri tangazo la kwenye gazeti la serikali," alisema Mahera.

"Baada ya tangazo la kuvunjwa kwa Bunge, tarehe ya kufanyika kwa uchaguzi itatangazwa kati ya siku tano hadi 25, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kifungu 37(1), kinaielekeza Tume kufanya uteuzi kwa wagombea nafasi ya kiti cha urais, ubunge na udiwani," alisema Mahera.

Pia Mahera alisema, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kifungu cha 46(1), kinasema kuwa tarehe ya uteuzi wa wagombea itatakiwa kutajwa ndani ya siku 60 hadi 90 sambamba na kutangaza siku ya uchaguzi.

Alisema, kabla ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kufanya uteuzi, vyama vya siasa vinaweka utaratibu wa kuwapata wagombea kwa nafasi ya urais, ubunge na udiwani.

Alisema Tume itawateua wagombea wa nafasi ya udiwani kwa kuwa mgombea atatakiwa kujaza fomu namba 8(c) na kugongewa muhuri na Katibu Kata, Katibu wa chama ngazi ya jimbo au mkoa.

Kwa wabunge, vyama vitatakiwa kupeleka utambulisho uliogongwa muhuri kutoka ngazi ya jimbo, pia wagombea urais watapokea majina ya wagombea kutoka kwa vyama vya siasa vilivyowadhamini na fomu zao zitatakiwa kugongwa muhuri na makatibu wa vyama hivyo ngazi ya taifa.

Mahera aliwataka wananchi kujitokeza kuhakiki na kurekebisha taarifa zao katika Daftari la Wapigakura, ili wapate haki ya kikatiba ya kuwachagua viongozi wanaowahitaji.

"Nawaomba wananchi wajitokeze kwa wingi kuhakiki na kurekebisha taarifa zao katika Daftari la Wapigakura, pia nawaomba watunze kadi zao ili wapate fursa ya kuchagua viongozi makini watakaowaletea maendeleo," aliongeza.

Kadhalika, alisema uchaguzi wa mwaka huu, utakuwa uhuru na haki na kuwataka wananchi kujitokeza kupiga kura.

"Tume ipo kwa mujibu wa Katiba ya nchi ya mwaka 1997, ibara ya 74(6), imeonyesha majukumu yake ikiwamo kuratibu, kusimamia uchaguzi na kuandikisha wapiga kura kwa kiti cha urais, ubunge na udiwani.

"Bunge limetunga Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura 343 inaelekeza kuhusu uchaguzi na sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa namba 292 na madiwani," aliongeza.

Alisema ibara ya 74(11, 12 hadi 14), inaelekeza kwamba Tume hiyo, itakuwa huru katika kutekeleza majukumu yake bila kuingiliwa na mtu au chama chochote kwa kuwa ipo kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

## HABARI KITAIFA

# Afungwa miaka 30 jela kwa kubaka

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Sumbawanga imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela mkazi wa kitongoji cha Kizwite mjini Sumbawanga mkoani Rukwa, Samson Venance (27), baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kumbaka msichana mwenye umri wa miaka 18.

Pia mtuhumiwa anatakiwa kulipa faini ya kiasi cha Sh. 3,000,000 kwa kutenda kosa hilo kinyume cha sheria.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Jacob Ndira, alitoa hukumu hiyo jana baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa mahakamani na upande mashitaka ukiongozwa na wakili wa Serikali, Simon Peres.

Upande wa mashtaka uliieleza mahakama kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo Januari 17, mwaka huu majira ya usiku katika kitongoji cha Kizwite ambako ndiko yaliko makazi yake.

Ulidai mbakaji alienda nyumbani kwa binti huyo ambaye wazazi wake hawakuwapo nyumbani hapo na kumgongea mlango alipofungua alimkamata kwa nguvu na kuanza kumbaka.

Ilidaiwa kuwa muathirika alipiga kelele za kuomba msaada ndipo baadhi ya majirani walijitokeza na kumsaidia kwa kumkamata kijana huyo na kutoa taarifa Polisi ambapo askari walifika eneo la tukio na kumtia nguvuni Venance.

Awali Venance aliposomewa alikana kutenda kosa, lakini alitiwa hatiani baada ya upande wa mashtaka kutoa ushahidi wake ikiwemo kutoa vipimo vya hospitali vilivyoonyesha kwamba kitendo hicho kilifanyika.

Alipopewa nafasi ya kujitetea, aliiambia Mahakama kuwa siku hiyo alikuwa amelewa, hivyo hakumbuki alichokifanya.

Hakimu Ndira alisema kuwa kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo pasipo kuacha shaka, Mahakama hiyo imemkuta na hatia Venance kupitia kifungu Namba 130, kifungu kidogo cha kwanza na cha pili (E).

Pia Kifungu cha 131, (I) Sura ya 16, kanuni ya Adhabu kama ilivyofanyiwa Marekebisho mwaka 2020, hivyo inamhukumu kwenda jela miaka 30 na kulipa faini ya Sh. 3,000,000.

# Mamia wajitokeza kumdhamini JPM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMIA ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma wamejitokeza kumdhamini mgombea urais kwa tiketi ya chama hicho katika uchaguzi mkuu, Rais John Magufuli.

Rais Magufuli juzi asubuhi, alichukua fomu ya kutetea nafasi yake na kuipeleka kwa Katibu wa CCM, Mkoa wa Dodoma ili kumsaidia kutafuta wadhamini ndani ya chama.

Miongoni mwa wanachama hao ni pamoja na mamalishe, vijana, wajasiriamali, wanavyuo na waendesha bodaboda.

Akizungumza baada ya kuyapokea makundi hayo, Katibu huyo, Jamila Yusuph, alisema Rais Magufuli, amewakabidhi fomu yake ili kumsaidia kutafuta wadhamini.

Alisema, fomu hiyo inatakiwa kusainiwa na wadhamini 250, hivyo wanachama wanaohitaji kumdhamini, wanatakiwa kufika katika ofisi hiyo ili kupata fursa hiyo.

"Kwa kweli mhweshimiwa Rais, ametushtukiza, hakuna aliyekuwa anafahamu ujio wake, lakini na sisi kama chama lazima tuonyeshe kuwa hatutamwangusha kwa kujitokeza kwa wingi kumdhamini, lakini hata katika uchaguzi kumpigia kura nyingi na mkoa wetu uwe namba moja kwa wingi wa kura za urais," alisema.

Naye mwakilishi kutoka kundi la machinga, John Ndahani, alisema wana mdhamini Rais Magufuli kutokana na utendaji wake katika kipindi cha miaka mitano ya awamu yake ya kwanza.

Alisema, wamepata mkombozi kwa kuwa katika utawala wake walifanya kazi bila usumbufu tofauti na ilivyokuwa kabla ya utawala wake.

"Katika uongozi wa Magufuli, tumefanya biashara bila usumbufu hakuna mtu aliyetusumbua kutokana na kila mmoja wetu kupatiwa kitambulisho kwa gharama nafuu ya Sh. 20,000 kwa mwaka," alisema Ndahani.

Naye Hawa Mbogoni, mwakilishi wa kundi la mamalishe alisema mgombea wao, ni mmoja ndani ya chama na ambaye ni Rais Magufuli, na wanapendekeza wanachama wengine wasijitokeze kumpinga.

"Tunapenda Magufuli apite bila kupingwa, ili aitetee nafasi yake mwenyewe bila kupingwa na mwana CCM yeyote, ili amalizie awamu yake ya pili na kutuletea maendeleo zaidi ya haya," alisema.

Mwakilishi kutoka wanavyuo wa mkoa wa Dodoma Jackson Mathias, alisema kuwa wameamua kumdhamini Rais Magufuli pamoja na kumchangia kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kulipia fomu yake.

"Sisi katika awamu hii ya Magufuli kama wanachuo tumesoma kwa raha sana kwani mikopo yetu imekuwa ikiingia kwa wakati na hakuna migomo tena sasa tumeona kiasi kidogo cha fedha zetu za chakula tumchangie ili aweze kulipia fomu yake wakati huu anapojipanga kutetea nafasi yake," alisema.



Mwendesha guta akiwa amepakia mizigo na abiria juu katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA.**


## JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER.

**DEBT COLLECTIONS & AUCTIONEERING**

**HEAD OFFICE –Buzuruga plaza 2nd Floor Room No. 207 Mwanza**

**P.O BOX 11126 MWANZA, 0713/0789/0768-203040, josinacompany@gmail.com,josinacoltd@gmail.com**

### TANGAZO TANGAZO TANGAZO

JOSINA COMPANY LIMITED KWA AMRI TULIYOPEWA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA ,MKOA WA MWANZA, ITAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA NYUMBA, KWA TAREHE KAMA ILIVYO PANGWA KATIKA JEDWALI NA MUDA NI KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA.MNADA UTAKUWA **TAREHE 26/06/2020.**

| JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| DOTO KILEKA | NYUMBA-PLOT NO 82 BLOCK H"MAGU | MAGU-MJINI | 26/06/2020,SAA NNE ASUBUHI | JOSINA CO LTD |
| VALENCE M.MAHENGE | NYUMBA-PLOT 311 BLOCK B"NYEGEZI | NYEGEZI – STENDI KUBWA | 26/06/2020,SAA NNE ASUBUHI | JOSINA CO LTD |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. DHAMANA ZITAUZWA KAMA ZILIVYO, MNUNUZI ATALIPIA 25% YA BEI YA MNADA. 75% ITALIPWA NDANI YA SIKU 14 KUTOKA SIKU YA MNADA. AKISHINDWA KULIPA, MALIPO YA AWALI HAYATARUDISHWA.
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI ZA UMILIKI ZITAKUWA JUU YA MNUNUZI.
3. UKAGUZI WA DHAMANA ZINAZOUZWA UTAANZA SIKU MOJA KABLA YA MNADA.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**
**MKURUGENZI Josina Co. Ltd: 0768 203 040, WHATSAPP NO: 0713 203 040**



## Enabel Belgian Development Agency

**PRE-BID MEETING FOR UPCOMING CONSTRUCTION TENDERS**

Enabel, the Belgian Development Agency, through Water Sanitation and Kigoma Region Project (WASKIRP) plans to engage contractors and consultants for construction of water supply networks in Kigoma region. Several tenders are currently being prepared for publishing. Enabel therefore has organized a meeting for interested contractors and consultants for orientation to the bidding documents and processes so as to achieve appropriate responsiveness to the tenders. The meeting will be held as follows:

**Date** : **Saturday, 27 June 2020**
**Venue** : **Hotel Slipway, Slipway Road, Msasani Peninsula, Dar es Salaam**
**Time** : **10:00 – 14:30 PM**

The meeting will allow a maximum of 2 people per company. Interested companies are encouraged to submit their interest and names of their representatives by Thursday, 25th June 2020. No company will be allowed to be represented in the meeting if they fail to register their interest to attend the meeting and if they do not submit their names before this date.

In the wake of the COVID 19 situation, the meeting will adhere to strict preventative measures as guided by the government for such meetings. All participants are required to bring facial masks to wear while the organizers will ensure availability of sanitization fluids and hand washing facilities.

Submit your interest to participate in the meeting and the name(s) of your company representative through email to **constantin.hien@enabel.be** copying to **lilian.ayo@enabel.be**

215780102

# Kesi 23 rushwa ya ngono zafunguliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imefungua majalada 23 ya kesi za rushwa ya ngono, kumi kati ya hizo zikisikilizwa na tano kushinda katika mikoa mbalimbali.

TAKUKURU pia, imewataka wakuu wa vyuo kusimamia suala la rushwa ya ngono vyuoni ili kusaidia kupunguza ukandamizaji unaofanywa hususani kwa watoto wa kike.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye uzinduzi wa kampeni ya 'Vunja ukimya kataa rushwa ya ngono', Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema kila Mtanzania ana haki ya kutoa taarifa anapoona kuna viashiria vya rushwa ili izifanyie kazi na kutokomeza.

Alisema rushwa ya ngono ni tatizo kwa jamii na kazi yao ni kuisimamia na kuhakikisha wameitokomeza ili wanafunzi wasome kwa raha badala ya karaha kama ilivyo kwa wanafunzi wa kiume.

"Naomba watu tutumie huu mtandao wa vunja ukimya ili kusaidia kutoa taarifa, tunahitaji kuona kila mwanafunzi anakuwa na amani katika masomo yake," alisema Brigedia Jenerali Mbungo.

Kadhalika, alisema TAKUKURU, imejipanga kwa kushirikiana na Mfuko wa Wanawake nchini (WFT), kuhakikisha wanapiga vita hiyo rushwa ili wanafunzi waweze kusoma kwa amani na sio kukarahishwa na vitendo vya rushwa kila kukicha.

Alisema anawapongeza WFT, kutokana na kuonyesha ushirikiano mzuri wa kufanikisha kupinga vita rushwa ya ngono vyuoni.

Akizungumzia majalada yaliyofunguliwa ya kesi za rushwa alisema, yanaendelea kusikilizwa huku mengine yakionyesha kumalizika na kwamba watakuwa tayari wakati wowote kutoa msaada mtu anapokutana na vikwazo vya rushwa hususani kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

Hata hivyo, alisema kuna ripoti ya utafiti wa kisayansi ambazo zitasaidia kupata kila kitu kuhusu rushwa ya ngono, na huo ni mkakati ambao umewekwa katika taasisi za elimu.

Prof. Rukia Meena kutoka WFT, alisema mtizamo wa chuo utabadilika endapo wakuu wa vyuo watakuwa mstari wa mbele kupiga vita rushwa ya ngono ambayo imekuwa ikiwapasua vichwa wanafunzi.

Alisema wanafunzi wengi wanatoa malalamiko yao vyuoni na kuwataka wakuu wa vyuo kuwa mstari wa mbele kuwasikiliza na kuyafikisha sehemu husika ili yaweze kufanyiwa kazi na kutolewa uamuzi.

Alisema wanataka kuona wanafunzi wanasoma bila vikwazo vyovyote kutoka kwa wakufunzi wao jambo ambalo hivi sasa linapigiwa kelele.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kulia), akimtwisha ndoo ya maji, Kibibi Elias, baada ya kuzindua mradi wa maji katika kijiji cha Uzogole Ibadakuli, mjini Shinyanga jana, uliotekelezwa na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), kwa gharama ya Sh. milioni 88.8, ili kuwaondolea adha ya kutumia maji ambayo siyo salama kwa afya zao. **PICHA: MARCO MADUHU**

# JPM akemea Suma JKT kunyanyasa raia

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amewataka Suma JKT wanaolinda maeneo mbalimbali vikiwamo vituo vya mabasi, kuacha tabia ya kurusha watu vichura na watakaobainika kufanya hivyo waondolewe.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, kwa njia ya simu mbele ya wafanyabiashara wa stendi ya mabasi ya Dodoma.

Alisema anataka Suma JKT wawahudumie watu na siyo kuwarusha vichura na kueleza kuwa hataki kuona wananchi wanafanyiwa hivyo kwenye nchi iliyo huru.

"Tulipata uhuru mwaka 1961 kwa hiyo kwa hilo nimekubaliana na wafanyabiashara hao sitaki watu warushwe vichura," alisisitiza.

Katika mazungumzo hayo, Rais Magufuli alitaja jambo ambalo hajakubaliana na wafanyabiashara hao ni kuhusu wapigadebe ambao wakati mwingine baadhi yao hugeuka kuwa wezi.

"Kwenda pale kituoni kupiga debe hapana, kapige debe nyumbani kwako, kupiga debe pale siyo ajira nzuri, ajira nzuri ni watu kufanyabiashara kama wana zabibu, karanga huo ndiyo ujasiriamali.

Alimwagiza Mkurugenzi wa jiji hilo, kuhakikisha anatengeneza vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo.

"Shirikiana nao na umeonyesha wewe ni kijana mzuri unayependa maendeleo kwa ajili ya jiji la Dodoma. Hakikisha vijana wanapata mikopo ambao serikali huitoa wa asilimia nne.

"Mikopo ya wanawake asilimia nne, ya watu wenye ulemavu asilimia mbili, jiji lako linajitahidi kwenye makusanyo mazuri, hebu wape mikopo hao vijana, ninataka wafanikiwe katika maisha yao."

# Jafo asitisha uuzaji eneo la kijiji

**Na Augusta Njoji,** BAHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amekerwa na kuagiza kusimamishwa mchakato wa uuzwaji wa eneo la Kijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa lenye ukubwa wa hekari 200.

Mchakato huo ulikuwa wa kuliuza kwa raia wa kigeni, hivyo Jafo amefanya uamuzi huo ili kubaini uhalali wa uuzwaji wake.

Jafo alitoa agizo hilo wilayani Bahi wakati akizindua Shule ya Sekondari ya Kata ya Nondwa iliyojengwa na halmashauri hiyo kwa kutumia mapato yake ya ndani.

Alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loatha Sanare, kusimamisha mchakato huo na suala hilo lifanyike kwa kushirikisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

"Haiwezekani mchakato ufanyike bila ya kushirikisha wananchi wa kijiji husika na uchunguzi huu uangalie uhalali wa muuzaji na mnunuaji pia kujua dhamira waliyokuwa nayo," alisema.

Aidha, alisema timu hiyo iangalie kulikuwa na uhalali gani wa kuuza mali hiyo na mnunuaji pia aangaliwe kama hakuna harufu ya rushwa.

"Raia wa kigeni, huyu aliyependekeza kuuzwa alishawishiwa na nini, na tangu lini mgeni akamiliki ardhi nchi?" alihoji Jafo.

Hata hivyo, alisema Baraza la Madiwani katika kikao chao cha mwisho lilipitisha uamuzi wa kuuzwa eneo la kijiji lenye hekari 200 bila kuwashirikisha wananchi pamoja na kwamba Mkuu wa Mkoa aliwaandikia barua ya kuzuia wasifanye hivyo.

"Hivi huu ni udhaifu wa hali ya juu wa madiwani ambao katika kikao chao cha mwisho cha kuvunjwa baraza lao ndio waliidhinisha hili," alisema na kuendelea:

"Hili eneo ambalo limeuzwa kwa Mchina linatumika na Wachina kutekeleza miradi ya miundombinu ya majengo ambayo wangeweza kuyabadili kuwa kituo cha afya au zahanati."

"Yaani sijui waliuza ili wapate hela za kuwalipa madiwani viinua mgongo vyao na madeni mengine, hii ni tabia mbaya, nimechukizwa sana," alisisitiza Jafo.

# Ashikiliwa kwa tuhuma za rushwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wilaya ya Rufiji, mkoani Pwani, inamshikilia Salum Mkemi, mkazi wa Dar es Salaam na mwenyeji wa wilaya hiyo kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana mjini hapa, Mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Pwani, Suzana Raymond alisema, Mkemi anashikiliwa kwa lengo la kufanya uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili.

Alisema, uchunguzi wa awali wa TAKUKURU umebaini kwamba mtuhumiwa amekuwa akidaiwa kutoa fedha na kufanya vikao na baadhi ya wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM wilayani Rufiji.

Mtuhumiwa huyo pia anadaiwa kufanya kampeni kabla ya muda kuelekea uchaguzi mkuu wa viongozi uliopangwa kufanyika mwezi Oktoba, mwaka huu.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za watu wanao jihusisha na vitendo vya rushwa katika maeneo yao.

Mkuu huyo wa TAKUKURU alitoa wito kwa wananchi wa Rufiji kukataa kurubuniwa na watu wachache wasio na nia njema na nchi yao.

## HABARI KITAIFA

# CCM yatoa madai mazito jimbo la Sugu

**Na Emmanuel Lengwa, MBEYA**

JOTO la uchaguzi Mkuu wa madiwani, wabunge na Rais limeanza kupanda mkoani Mbeya baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoa madai mazito ya kuwapo makada wake ambao wameingiza kiasi kikubwa cha fedha kutoka nje ili kuhakikisha chama hicho kinashindwa kwenye uchaguzi huo hasa katika Jimbo la Mbeya Mjini.

Madai hayo yametolewa na Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa CCM, Bashiru Madodi, akiwa kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Mbeya jijini Mbeya.

"Tunajua kwamba kuna fedha kutoka nje ya Mkoa wa Mbeya zimeingizwa ili kuhakikisha kuwa CCM inashindwa uchaguzi hapa Mbeya Mjini, tunajua kuwa kuna wana- CCM wenzetu wameanza vikao vya siri kuwasaidia wapinzani ili washinde, niwahakikishie kuwa mwaka huu hatutawavumilia," alidai bila kutoa uthibitisho.

Madodi aliwaagiza Wenyeviti wa CCM ngazi ya Wilaya pamoja na kamati za Siasa za Wilaya kuorodhesha majina ya wanachama wa CCM ambao wameanza vurugu za kujipitisha kwa wanachama kuomba kupigiwa kura ili wapate nafasi ya kuteuliwa kugombea ubunge na udiwani kwenye maeneo yao na kuyafikisha ofisi ya CCM mkoa ili hatua kali dhidi yao zichukuliwe.

Alisema kuwa CCM inazo taratibu zake za kufanya uteuzi wa wagombea hivyo ikitokea mwanachama anakiuka taratibu hizo ni lazima hatua kali zichukuliwe dhidi ya mwanachama huyo kwa nia ya kulinda katiba, kanuni na miongozo ya chama.

"Hata sisi ngazi ya Mkoa tumeanza kuorodhesha watu ambao wameanza fujo mapema kwa ajili ya uchaguzi na hata ninyi viongozi wa CCM ngazi ya Wilaya andikeni majina ya watu wa aina hiyo na kutuletea ili tuwashughulikie kwa mujibu wa taratibu za chama chetu," alisema Madodi.

Aliongeza kuwa, uzoefu unaonyesha baadhi ya wanachama wa CCM hasa katika Jimbo la Mbeya Mjini wasipoteuliwa kugombea nafasi za uongozi hukisaliti chama na kwenda kuwasaidia wapinzani, jambo ambalo kwa mwaka huu haliwezi kuvumiliwa hata kidogo.

Madodi alisema kuwa ikitokea mwanachama yeyote wa CCM akahisiwa au kubainika kuwa anashirikiana na wapinzani kukihujumu chama kwenye uchaguzi Mkuu ujao, atasimamishwa uanachama na baada ya uchaguzi kumalizika atashughulikiwa.

"Tukikubaini kuwa unakihujumu chama kwa kushirikiana na wapinzani wakati wa uchaguzi, tutakachokifanya kwanza ni kukusimamisha uanachama kwanza ili utupishe sisi tuendelee kukipigania na baada ya uchaguzi tutarudi kukushughulikia na niwakumbushe tu kwamba hakuna kosa kubwa kama kukifanya chama kinuke mbele ya watu au kukihujumu kwenye uchaguzi, adhabu yake ni kufukuzwa uanachama," alisema Madodi.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Solomon Itunda alisema kuwa mazingira ya uchaguzi Mkuu ya mwaka huu ni tofauti na yale ya mwaka 2015 hivyo CCM ngazi ya Mkoa imejipanga kuhakikisha inawafuatilia wanachama wote ambao watathubutu kukisaliti chama na kwenda kuwasaidia wapinzani.

Alisema kuwa chama kimeweka mikakati ya kuhakikisha CCM inashinda jimbo la Mbeya Mjini na kwamba yeyote atakayejaribu kuvuruga mikakati hiyo atashughulikiwa ipasavyo.

"Tumejidhatiti kimkakati kuhakikisha CCM inashinda uchaguzi hapa Mbeya Mjini, kwa mwanachama wetu atakayejaribu kuvuruga mikakati yetu hatutamvumilia na hakuna jiwe litabaki juu ya jiwe maana yote tutayapindua," alisema Itunda.



Meneja wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Mkoa wa Arusha, Ladislaus Bamanyisa (kulia), akimwonyesha Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula (mwenye miwani), sehemu ya eneo la mradi wa Safari City-Arusha, wakati wa ziara ya kukagua miradi inayoendeshwa na shirika hilo, mkoani Arusha jana. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqqaro. Habari Uk. 9. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wazazi, wamiliki wa shule wavutana kuhusu ada

**Na Romana Mallya**

WAKATI serikali ikitoa mwongozo kwa shule zinazotarajia kufunguliwa Juni 29, baada ya kupungua maambukizi ya virusi vya corona, wamiliki wa shule na wazazi wameanza kuvutana kuhusu ulipaji ada.

Nipashe imeona barua za baadhi za shule binafsi zikielekeza wazazi kulipa ada ya muhula wa pili ambao wanaulalamikia kuwa watoto wao hawakusoma kutokana na janga la corona.

Katika barua ya baadhi ya shule wilayani Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam, iliyoandikwa jana na meneja wa shule kwenda kwa wazazi, iliwajulisha kuwa ili kufidia muda ambao watoto walikaa nyumbani, waraka uliotoka umeagiza kwamba wazazi wanatakiwa kulipa ada ya muhula wa pili.

"Ili kufidia muda ambao watoto walikaa nyumbani, waraka uliotoka umeagiza wanafunzi watarejea shuleni Juni 29 na kumalizia muhula wa kwanza wa masomo hadi Agosti 28, na kuanza muhula wa pili ambao utaisha Desemba 18, na muda wa masomo kwa siku uongewe kwa masaa mawili," ilieleza.

Pia barua hiyo iliwaeleza wazazi kuwa kutokana na agizo hilo, wanafunzi wa shule hiyo, watakuwa wanaanza masomo asubuhi kama kawaida na kuendelea hadi saa kumi na moja jioni badala ya saa tisa alasiri.

"Ulipaji wa ada utakuwa kama ifuatavyo, muhula wa pili malipo yafanyike kabla ya Juni 29, muhula wa tatu malipo yafanyika kabla ya Septemba Mosi na muhula wa nne malipo yafanyike kabla ya Novemba Mosi,"

Kutokana na mkanganyiko huo, uongozi wa shule ulifafanua kuwa kwenye muhula wa pili ambayo wazazi wanaulalamikia, zipo wiki mbili za likizo fupi.

"Zipo wiki mbili nyingine za likizo fupi za mwezi Septemba na wiki tatu ambazo zimeongezwa na Waziri za mwezi Desemba hizo hawajaziona, wazazi tumeshawaelewesha," alisema.

Alisema kwa mujibu wa Waziri, hakuna muda uliopotea kwa sababu ameongeza hadi saa za kufundisha.

"Ule muda ulioliwa na corona, Wizara ya Elimu umeufidia ndiyo maana tutafunga shule mwezi Desemba baada ya kuongezwa wiki tatu, kwa hiyo muda ambao umeongezwa wataulipia," alisema.

Aidha, wazazi walilalamikia uamuzi wa kuwataka kulipa fedha ya usafiri na chakula ambacho wanafunzi hao hakutumia kwa muda wote waliokuwa nyumbani.

"Mnataka tulipe ada bila ufafanuzi, je malipo ya usafiri na chakula yanalipwa kwanini?wakati wanafunzi alikuwa nyumbani tangu Machi 16?" alihoji mmoja wa wazazi kwenye kundi cha shule.

Jana Nipashe ilishindwa kuwapata viongozi wa Umoja wa Wamiliki wa shule binafsi. Mmoja wa viongozi aliyepatikana, aliahidi kulitafuta gazeti hili, lakini hakufanya hivyo hadi tunakwenda mitamboni.


**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**DAVID REUBEN MSHUZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 563 BBF** yenye chasis namba **ACA210047595** injini namba **1AZ0162837.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: **IR/TR/RB/11134/2020**

115780202



**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA**

TPA

**TAARIFA KWA UMMA**



**MWENYE PICHA HAPO JUU NI BWANA MADARAKA ROBERT MADARAKA ALIYEKUWA MWAJIRIWA WA MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA) KATIKA BANDARI YA KIGOMA AMEFUKUZWA KAZI KWA KOSA LA UTORO NA BILA YA KUKABIDHI OFISI UNAOHUSISHWA NA MAKOSA MENGINE ALIYOYATENDA KWA KUSHIRIKIANA NA WAFANYAKAZI WENZAKE NA HATUA ZA KINIDHAMU NA KISHERIA ZINACHUKULIWA.**

**KWA YEYOTE ATAKAYESAIDIA KUTOA TAARIFA ZA KUPATIKANA KWAKE ZAWADI NONO ITATOLEWA. TAARIFA HIYO ITOLEWE KWA MKURUGENZI MKUU TPA SIMU NAMBA +255 22 2116250 AU KATIKA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU YAKO.**

**IMETOLEWA NA MKURUGENZI MKUU TPA**

2157812O2

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tufanye utafiti zaidi likizo ya corona

**NI** taarifa nyingine za kusikitisha wazazi na walezi zinazotokana na unyanyasaji wanaofanyiwa mabinti, baada ya ripoti za hivi karibuni kueleza kuwa katika kipindi cha likizo ya corona mabinti zaidi ya 100 walipata ujauzito.

Ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu cha Dar es Salaam (LHRC).

Mimba ni jambo moja lakini utumikishwaji haramu wa watoto nalo ni jambo jingine kwa hiyo huenda nao umeendelea kushamiri wakati wa kipindi cha likizo ya corona.

Ni wazi kuwa watoto wenye umri wa kati ya miaka 7 hadi 17 ambao walikuwa likizoni wameathirika hasa vijijini na hata mijini kwani wametumikishwa kwenye ajira za kulima, kupanda, kunyunyiza dawa kwenye mashamba ya mazao mbalimbali pengine ya tumbaku.

Watoto hawa huenda wamesafirishwa kutoka mikoa mbalimbali au ni wenyeji wa vijijini ukulima huo unapofanyika.

Unyanyasaji watoto huwatumikisha kwenye kazi mbalimbali za kilimo bila kujali ajira zao licha ya kwamba wanaoumizwa zaidi ni watoto wa kiume.

Kwa hiyo ni wazi kuwa watoto hao watakuwa wametumika kupalilia, kupanda , kutunza kama kunyunyuzia dawa, kuvuna na pengine kukausha mazao kama tumbaku.

Wahusika wamewatumia watoto kwasababu wanafahamu kuwa hawaelewi mambo ya mshahara wala haki zao hivyo imekuwa rahisi kuwanyonya na kuwanyanyasa hasa wale wanaotoka katika familia maskini au zile za wasiojiweza au yatima na wanaojilea wenyewe.

Licha ya kutumikishwa kwa kazi ngumu pengine kulima, kupalilia, kuweka kemikali za kuua wadudu, kupanda na kuweka mbolea za kupandia na kukuzia pamoja kuvuna huenda wako wengine ambao hawakupata haki zao.

Mbali na kilimo wapo wanaotumikishwa kukata magogo na kuni, kusaidia kazi za kufuga kama wanyama wakiwamo ng'ombe, nguruwe na mbuzi.

Watoto hawa wameumizwa kwa sababu wanaowatumikisha siyo waadilifu linapokuja suala la malipo huenda wanawahadaa kuwa hawajapata mavuno au hawana fedha hivyo wengi watakuwa wameambulia hasara na wametoka tupu.

Tunaona kuwa watoto hawa wana umri mdogo hivyo wanaathirika na dawa na kemikali za sumu pamoja na kazi ngumu zinazofanyikwa kwenye kilimo hivyo kuhatarisha maisha yao, licha ya kwamba kuna jamii na familia zinazowaruhusu kufanyakazi.

Hivyo, kwa namna ambavyo kituo cha HLRC kimeangalia tatizo la ujauzito ndivyo pia wengine wachunguze kutumikisha watoto kwenye migodi na maeneo mengine hatarishi ambayo kazi zake hazikustahili kwa watoto hao wadogo.

Pamoja na kulima kuchimba madini na mambao mengine wadau wengine kama LHRC wasaidie kuchunguza kazi nyingine kama kuwapeleka watoto msituni kukata magogo na kuchuma mkaa.

Hayo ni mambo yanayoweza kufanyika katika ukanda wa pwani na sehemu zenye misitu.

Tunaona kuwa ni vyema pia kufanya uchunguzi katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita na Shinyanga, ambako familia zinalima, kufuga, kuchimba madini pamoja na kukata mkaa.

Kwa sababu utafiti umeangalia waliopata mimba mwingine uelekeze pia jicho kwenye wanaotumikishwa kwenye ajira nyingi nyingine mbovu. Hili si jukumu la LHRC pekee ni vyema pia Idara za Ustawi wa Jamii na wadau wengine wa kiserikali zikiwamo kama za elimu vijijini wakafuatilia ili wahusika wanapogundulika wachukuliwe hatua.

Ni wazi kuwa bila kuwa na mikakati watoto waliotumikishwa wanaendelea kuwa kwenye hatari ya kubakwa, kulawitiwa hata kuathirika kisaikolojia na kimwili.

Hongera LHRC, tunaomba na wengine waige mfano wenu kusaidia kuwalinda watoto wa Tanzania ambao ndiyo uti wa mgongo wa taifa la kesho..

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wekeni sawa ya muhimu, Wamachinga mtawapata



Na Sabato Kasika

**KUNDI** la wajasiriamali Wamachinga wanatajwa kuwa ndiyo wanaoleta muunganiko wa watu katika kada mbalimbali, wakiwamo wasomi wenye elimu ngazi tofauti; shahada, astashaada, kidato cha sita na cha nne, darasa la saba na wasiopiga hatua shuleni.

Wote wanaunganika na kufanya biashara kwa ngazi ya Wamachinga, kwamba kati ya Watanzania milioni 50, walioajiriwa serikalini na sekta ya umma ni 520,000.

Hivyo, kundi kubwa ni la watu ambao ama wamejiajiri au wameajiriwa katika sekta binafsi, kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo.

Anasema, kundi kubwa ni la wanaojishughulisha kutafuta riziki zao wenyewe, ambazo ndiyo asilimia ya wanaoangukia katika kundi la Wamachinga.

Wakati alipofungua Mkutano Mkuu wa Shirika la Umoja wa Wamachinga Tanzania (Shiuma), jijini Dodoma, Jafo aliwaagiza wakuu wa wilaya nchini kuzisimamia halmashauri zilizo chini ya mamlaka zao za utawala, kutenga maeneo maalumu ya wafanyabiashara wadogo.

Lengo la maagizo hayo ni kuwawezesha kuendesha shughuli zao bila kuvunja sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na serikali, hivyo viongozi wana wajibu wa kuratibu na kuhakikisha maeneo ya Wamachinga kufanya biashara.

Ni mandhari yanayotengwa na halmashauri mbalimbai na kimsingi kwamba, uchumi jumuishi unaweza kupatikana kupitia urasimishaji wa sekta isiyo rasmi, ili itoe mchango, pale inapotambuliwa ni sehemu muhimu katika ukuzaji uchumi wa nchi.

Hatua za kutambua mchango wa sekta isiyo rasmi hasa kwa wafanyabiashara hao wadogo zinazochukuliwa na mamlaka husika zinaweza kuchangia uchumi wa nchi na kuongeza ajira zaidi.

Kasi ya kuwatengea maeneo ingeongezwa ili wahamie huko kuliko ilivyo sasa, kwani wengi bado wanaendesha biashara kwenye mazingira yasiyo salama.

Mfano mmojawapo kwa jijini Dar es Salaam, Kimara Mwisho, katika barabara ya kuelekea Bonyokwa, wilayani Ubungo. Mahali hapo huwa wajasiriamali wanapanga bidhaa zao chini ya nyaya za umeme mkubwa, hali ambayo ni hatari kwa usalama wao.

Suala la kuwatengea maeneo rasmi ya biashara yenye huduma zote muhimu, linapaswa kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu, ili biashara hizo zifanyike kwa usalama zaidi, kwani nao wana mchango mkubwa katika ukuzaji uchumi wa nchi.

Wanaotumikia katika sekta isiyo rasmi, wanaweza kuimarisha soko la ajira na kuwawezesha kuwa na uhakika wa vipato katika shughuli zao za kila siku.

Ninaamini kwamba sekta isiyo rasmi hasa kwa wafanyabiashara wadogo, inabeba idadi kubwa ya watu na ajira, ambazo hazitoi mchango wa kodi, hivyo zikiboreshwa, zitachangia kuongezeka kwa idadi ya walipa kodi nchini.

Kuwatambua Wamachinga kama sehemu muhimu ya kukuza uchumi kwa kuwapa vitambulisho, ni hatua nzuri, pia suala la kuwapo makazi ya kufanyia shughuli zao kwa usalama ni nyeti.

Kilichofanywa jijini Dodoma, kinapaswa kuwa mfano kwa pengine, kwani jumla ya Wamachinga 200 waliokuwa wakifanya biashara holela na kuzagaa maeneo yasiyo rasmi ya stendi na pembezoni mwa soko la Sabasaba wamepewa eneo la biashara.

Ofisa Masoko wa jiji la Dodoma, James Yuna, anasema mtindo wa kufanya biashara holela ulikuwa unahatarisha afya na biashara zao, hata ikabidi watengewe eneo jipya kwa ajili ya shughuli zao.

Kwa ujumla ni kwamba, ukosefu wa maeneo ya kufanya biashara ni changamoto inayowakabili wafanyabiashara wadogo, licha ya uhalisia kwamba wameanza kutambuliwa na kupewa vitambulisho maalumu vya kiserikali.

Sasa niseme, wakati juhudi za kusambaza vitambulisho vya Wamachinga zikiendelea kama ambavyo mwaka huu Mkoa wa Mwanza umetoa vitambulisho vya 73,000 kwa awamu ya pili, suala la maeneo rasmi ya biashara linapaswa kutiliwa mkazo.

Waziri Jafo alishasema kwamba Wamachinga wanaleta muunganiko wa watu wa kada mbalimbali wanaofanya biashara kama wamachinga, hivyo hawana budi kufanya shughuli zake katika maeneo rasmi.

Jambo muhimu la kuzingatia katika hilo, ni kuwatengea maeneo rasmi, huduma zote za msingi kuanzia maji, vyoo, usafiri na vingine vingi vinavyohitajika ili kuwaondolea usumbufu usio na sababu.

Hicho ndicho kilio chao cha muda mrefu, ambacho Wamachinga wamekuwa wakikimbia walikopangiwa na kwenda maeneo mengine, sababu ni pale wanakuta hakuna huduma zote muhimu kwao.

## HABARI KITAIFA

# NMB yakopesha wakulima wa muhogo Handeni bil. 3/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetimiza azma ya serikali katika kupanua wigo wa huduma za kifedha pamoja na mikopo kwa wakulima wadogo nchini wanaojishughulisha na kilimo cha muhogo wilayani Handeni Mkoa wa Tanga.

Mkopo huo umepewa dhamana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili kuwezesha wakulima hao wadogo ili waweze kukopesheka kirahisi.

Akizungumza katika mkutano na wakulima hao katika eneo la Mkata Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga, Ofisa Mkuu wa Wateja Wadogo wa NMB, Filbert Mponzi, alisema mkopo hiyo itawanufaisha wakulima 421 ambao watakuwa katika makundi 43.

"Sh. billioni tatu ni fedha nyingi, hivyo mzitumie vizuri ili na wengine waweze kufaidika nazo. Huu ni uhamasishaji wa uwekezaji katika zao la muhogo ili kuwawezesha wakulima kujiongezea kipato na wakati huo kuendanana soko la China," alisema Mponzi.

Alisema wanaimani kubwa na TADB, ushirikiano wao umeleta mafanikio mazuri.

Alisema Benki ya NMB itaendelea kusaidia wakulima wadogo ili wainuwe kipato chao.

Akifafanua kuhusu aina ya riba hasa kwa vikundi, Mponzi alisema riba yake ni asilimia 16 na wanaokopeshwa ni wakulima wadogo walio kwenye vikundi.

Alisema kuwa kwa miaka kadhaa sasa kilimo kimekuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa Tanzania hasa katika upatikanaji wa chakula, biashara ya mazao nje ya nchi, kusaidia upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani na kutoa ajira kwa Watanzania.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe, aliishukuru benki ya NMB kwa mkopo huo kwa wakulima wa muhogo.


"Mkopo huu utaongeza tija katika kilimo cha muhogo kwa wakulima wa Handeni," alisema Gondwe.

Katika kutatua changamoto ya masoko ya zao hilo Mkuu huyo wa Wilaya hiyo amesema kuwa kiwanda cha kusindika zao hilo kinatarajiwa kuanza kazi miezi michache ijayo na taratibu zinaendelea ili kuweza kulipata soko la china.

Alisema kilimo cha zao la muhogo kimeongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia 87 mwaka huu na kipato kwa wakulima wilayani Handeni.

Akielezea harakati za wilaya ya Handeni katika kuhamasisha zao la muhogo, Mwenyekiti wa Umoja wa Wazalishaji na Wasindikaji wa Muhogo Tanzania (TACAPPA), Mwantumu Mahiza, alisema mkopo huo wa Sh. bilioni 3 ni historia kwa nchi ya Tanzania na ni uhamasishaji unaoenda sambamba na utoaji mafunzo, utoaji mbegu bora kwa wakulima pamoja na kuhakikisha kuwa kilomo cha muhogo kinaongeza tija.

Kwa mujibu wa Mahiza, sasa hivi zao la muhogo katika Wilaya ya Handeni limekuwa la kibiashara na hali hiyo inatokana na usafirishwaji wa muhogo mbichi kwa wingi kila siku kutoka wilaya hiyo kwenda Dar es Salaam.




Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe (kushoto), akipokea mfano wa hundi ya Sh. bilioni 3 kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na za Kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kulia), zilizotolewa na benki hiyo, kwa ajili ya vikundi 23 vyenye wakulima 421 wa muhogo wa eneo la Mkata. Katikati ni Mwenyekiti wa wakulima hao Tanzania, Mwantum Mahiza na wa tatu kulia ni Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# TAKUKURU yawaonya wagombea watoa rushwa

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewaonya wagombea wanaotumia rushwa kupata nafasi za uongozi.

Pia, imewaonya wananchi au wanachama wanaopokea rushwa kutoka kwa watu mbalimbali kuacha mara moja kwa kuwa taasisi hiyo iko macho muda wote.

Akizungumza kupitia kipindi cha Kumepambazuka kinachorushwa na Radio One, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU wilayani Temeke, Donasia Mkesi, alisema kumekuwa na baadhi ya wagombea wanaotoa rushwa kwa wananchi ili wachaguliwe.

Alisema TAKUKURU imepata taarifa za baadhi ya wagombea wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na wako macho kwa yeyote atakayebainika atakamatwa na kufikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

"Tumeanza kupokea malalamiko mengi kuhusu wagombea wanaopita pita kabla hata kipenga hakijapulizwa na wengine tumeanza kuwahoji na kuna ambao wamekimbia na kuacha baadhi ya vitu vyao kama fedha na magari," alisema Mkesi.

Aliongeza kuwa kuna wengine wamezuiliwa wakati uchunguzi ukiendelea na itakapobainì kuwa ni kweli wamejihusisha na vitendo vya rushwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Alisema kutokana na ushindani wa kisera na uchaguzi uliopo ndiyo sababu baadhi ya wagombea kujihusisha na rushwa ili wachaguliwe au kutetea nafasi zao. "Mgombea anapoona kuwa hana sera zinazoweza kuishawishi jamii ndipo anapotumia ushawishi wa kifedha, wengine wanafanya hivyo kwa tamaa za kutaka kujinufaisha mwenyewe," alisema Mkesi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, wananchi wanatahadharishwa kutowachagua wagombea wanaotoa rushwa kwa kuwa wakishapata madaraka watataka kurudisha fedha zao walizozitumia na kusahau kuleta maendeleo.

Alisema ni kinyume na sheria kwa wagombea kutoa fedha kwa wananchi wakati wa kampeni, uchaguzi na baada ya uchaguzi na TAKUKURU itakapo mbaini yeyote atakayejihusisha na hilo atachukuliwa hatua.

# Asilimia 61 ardhi hatarini kugeuka jangwa

**Na Faudhia Sultan,** UDOM

UTAFITI umebaini asilimia 61 ya ardhi Tanzania, ipo katika hatari ya kugeuka jangwa kutokana na utegemezi mkubwa wa rasilimali kama misitu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu, asilimia 16 ya nchi imekwisha onyesha dalili za wazi za kuwa jangwa.

Alisema hayo ikiwa ni Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame Duniani.

Maadhimisho ya mwaka huu yamebebwa na kaulimbiu, 'Tudhibiti Kuongezeka kwa Uzalishaji wa Chakula na Malighafi; Tukabiliane na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame'.

Taarifa ya waziri ilitaja sababu ya jangwa kuwa ni utegemezi mkubwa wa rasilimali kama misitu ambao umechangia kwa kiasi kikubwa tatizo hilo.

"Utafiti unaonyesha kuwa asilimia 85 ya Watanzania wanategemea kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia. Utegemezi huu husababisha upotevu wa hekta 372,000 za misitu kila mwaka," alisema Zungu.

Alisema juhudi nyingi zimefanyika ili kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame ikiwa ni pamoja na kuwapo kwa programu maalumu ya mpango wa kudhibiti ukame ya mwaka 2018.

"Utafiti wa kubainisha maeneo kame umeanza kufanyika nchi nzima; sheria, kanuni, miongozo, programu na matamko mbalimbali kwa kuzingatia sekta ambazo zina utegemezi wa moja kwa moja na ardhi.

Alitaja mipango na mikakati mingine ni kama mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji wa mwaka 2006, ambao unatekelezwa katika mikoa yote Tanzania Bara.

"Moja ya maelekezo ya mkakati huu ni kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka kwa kila halmashauri; Programu ya pili ya kuendeleza sekta ya kilimo (ASDP II 2017/18 - 2028/29) ambayo inatekelezwa nchi nzima.

"Uanzishwaji wa mashamba mapya ya miti ambapo jumla ya hekta 1,734 zimepandwa miti ya wino katika mikoa ya Songea, Iyondo Msimwa (Ileje) na Biharamulo (Chato)."

Alitaja maeneo mengine ni Mpepo (Mbinga), Buhigwe (Kigoma) na Mtibwa/Pagale (Mvomero).

Pia, alisema lipo shamba jipya kwa ajili ya uzalishaji wa gundi inayotokana na miti ya migunga lenye ukubwa wa hekta 50,000 lililoanzishwa katika Wilaya ya Iramba (Singida).

Waziri Zungu alisema katika kupunguza utegemezi wa nishati ya kuni na mkaa ambayo husababisha ukame na kuenea kwa jangwa, serikali ipo katika ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere Hydropower Station lenye uwezo wa kuzalisha megawati za umeme 2,115.

"Umeme huu utapatikana kwa bei rahisi na hivyo kuwezesha wananchi wa kawaida na taasisi kutumia umeme kama nishati ya kupikia," alisema.

Pia, kupunguza uzalishaji wa gesi joto unaosababisha mabadiliko ya tabianchi ambayo huchangia kuwapo kwa hali ya jangwa na ukame.

# Baba adaiwa kubaka watoto wake 3, mmoja apata ujauzito

**Na Ambrose Wantaigwa,** BUNDA

MKAZI wa Bunda (jina tunalo) anashikiliwa na polisi wilayani humo kwa tuhuma za kuwadhalilisha kijinsia na kuwabaka mfululizo watoto wake watatu, huku akidaiwa kumpa ujauzito mmojawapo.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, aliagiza kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo baada ya kutolewa taarifa na wasamaria wema kuwa vitendo hivyo vya udhalilishaji vimekuwa vikifanywa na baba huyo kwa muda mrefu.

Bupilipili alisema uchunguzi wa awali wa polisi ukibaini kuwa mtuhumiwa alijihusisha na matendo ya ubakaji kwa watoto wake, atafikishwa mahakamani haraka ili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Alivitaka vyombo vya uchunguzi kuharakisha usikilizaji wa kesi hiyo ili haki iweze kutendeka kwa watoto hao kwa wakati na iwapo mtuhumiwa akipatikana na hatia achukuliwe hatua kali za kisheria ili liwe fundisho kwa watu wenye tabia kama hiyo.

Mama mzazi wa watoto hao (jina linahifadhiwa), alidai baba huyo amekuwa akiwabaka watoto wake hao wakati yeye akiwa hayupo nyumbani na mara nyingi aliogopa kutoa taarifa kwa kuhofia kuvunjika ndoa yake.

Alisema kitendo cha hivi karibuni cha madai ya kumsababishia ujauzito mmoja wa watoto hao anayesoma darasa la tano, kilisababisha wasamaria wema hasa majirani kuingilia kati na kufanikisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo.

"Nilishangaa kuona mwanangu aliye na umri wa miaka 13 akibeba ujauzito na tulipomuuliza alisema alikuwa akishiriki tendo la ndoa na baba yake mzazi kwa kumlazimisha wakati mimi nikiwa katika shughuli za uzalishaji mali," alisema Gaudensia.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na kutetea haki za watoto na wanawake la Kivulini, Yassin Ally, vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vimekithiri katika baadhi ya jamii mkoani hapa kutokana na wanajamii kushindwa kutoa ushahidi mahakamani.

"Wengi wa waathirika wa matukio kama haya hasa maeneo ya vijijini wanaogopa kuripoti matukio hayo katika vyombo vya dola kwa kuhofia kuvunjika ndoa zao huku watu wa karibu wanaoshuhudia vitendo hivyo wakishindwa kutoa ushahidi mahakamni ili haki ipatikane kwa wakati," alisema Ally.



Mafundi wakiendelea na matengenezo ya chemba ya maji ya mvua katika ukarabati unaoendelea wa Barabara ya Shekilango, eneo la Sinza Madukani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mloganzila yatibu mawe kwenye figo bila upasuaji

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), tawi la Mloganzila, imeanza kutoa huduma za matibabu ya uvunjaji mawe kwenye figo na mfumo wa mkojo kwa kutumia njia ya mawimbi mshtuko bila kufanya upasuaji.

Huduma hiyo inafanywa kwa kutumia mashine inayotoa mawimbi sauti yanayosafiri kupitia ngozi hadi kwenye figo sehemu yenye jiwe au mawe na kuyavunja.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Miseru, alitangaza kuanza kwa huduma hiyo mpya katika hospitali hiyo jana, jijini Dar es Salaam, kuwa mawimbi yanayotumika hugeuka kuwa nishati yenye uwezo wa kuvunja mawe kuwa madogo mithili ya mchanga na kutoka kwa njia ya mkojo.

"Kuanzishwa kwa matibabu haya ni mwendelezo wa kutekeleza juhudi za serikali kuboresha huduma bobezi za kibingwa nchini ili kuongeza wigo wa huduma ambazo hapo awali zilikuwa hazipatikani nchini kutokana na kutokuwapo kwa wataalam, vifaa tiba au vyote na huduma hii inatolewa na wataalam wazawa wa MNH," alisema Prof. Museru.

Alisema huduma hiyo walianza kuitoa mwanzoni mwa mwezi huu na jumla ya wagonjwa 10 wamenufaika na matibabu hayo ambao pia hali zao zinaendelea vizuri.

Prof. Museru alisema faida ya matibabu hayo haihitaji mgonjwa kulazwa kwa sababu anaweza kutibiwa na kuruhusiwa kwenda nyumbani siku hiyo hiyo ili kuendelea na shughuli zake.

Alisema kuanzishwa kwa huduma hiyo kumesaidia kupunguza gharama walizokuwa wakitozwa wagonjwa kufuata huduma hiyo nje ya nchi kwa Sh. milioni 10, na hapa nchini wanatoa kwa Sh. 500,000.

Alifafanua kuwa, mgonjwa wa rufani anatozwa Sh. 500,000, binafsi Sh. milioni 1.2 na wagonjwa kutoka nje ya nchi watatozwa Sh. milioni 4.8.

"Kufuatia matibabu haya waliopatiwa ni wagonjwa 10, serikali imeokoa Sh. milioni 95," alisema Prof. Museru.

Kuhusu ukubwa wa tatizo Prof. Museru alisema kwa kipindi cha mwaka 2019 jumla ya wagonjwa 1,035 wenye mawe kwenye figo walionwa katika kliniki za wagonjwa wa nje MNH na kati ya hao wapya walikuwa 425 wakati waliolazwa kutokana na tatizo hilo walikuwa 14 na 50 walifanyiwa upasuaji wa kuondoa mawe kwenye figo.

Alisema pia katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2017 jumla ya wagonjwa 23 wenye matatizo ya mawe kwenye figo walipatiwa rufani ya kwenda nje ya nchi.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mfumo wa Mkojo, Dk. Isack Maro, alisema dalili za ugonjwa huo ni maumivu chini ya mbavu, kukojoa damu kama jiwe ni kubwa na limekwangua ukuta wa figo, maumivu wakati wa kukojoa kama jiwe limepata maambukizi ya bakteria na kukojoa usaha.

# Vyuo vikuu kusoma kozi ya diplomasia ya uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Diplomasia na Uhusiano wa Kimataifa (CFR) cha jijini Dar es Salaam, kimeanzisha kozi ya diplomasia ya uchumi kwa wahitimu wa vyuo vikuu.

Imeelezwa kuwa lengo ni kunyanyua na kuimarisha uwezo wa majadiliano katika masuala ya uchumi, hasa ya kimataifa kwa wafanyakazi katika balozi za Tanzania na watendaji katika sekta binafsi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mkurugenzi wa chuo hicho, Dk. Jeremia Ponera, alisema mafunzo haya yanaandaa wataalamu wa Tanzania kushiriki vizuri na kikamilifu katika utekelezaji wa azma ya taifa ya kujenga uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Kituo hiki, kama taasisi nyingine za umma, tumekuwa mstari wa mbele katika kutafsiri na kuunga mkono jitihada za serikali. Katika kipindi hiki ambacho serikali imeazimia kujenga uchumi wa viwanda ifikapo 2025, kituo kinawaandaa wataalamu ambao watasaidia kueleza fursa zilizopo kimataifa ili kufikia azma hiyo kwa haraka," alisema Dk. Ponera.

Alisema chuo hicho kimeisaidia Tanzania kuwaandaa mabalozi, wafanyabiashara za kimataifa katika kutambua fursa na kufanya majadiliano yenye tija kwa taifa. Chuo pia kimewasaidi mabalozi na wafanyabiashara kutambua umuhimu wa uwekezaji na kueleza fursa zilizopo Tanzania.

"Kama taasisi tupo katika nafasi nzuri ya kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuleta mageuzi katika ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda," alisema Dk. Ponera na kuongeza kuwa kila Mtanzania anapaswa kuunga mkono juhudi hizo kwa vitendo.

"Mbali ya kujikita katika kutafsiri malengo ya serikali kulingana na nyakati zilizopo, chuo kimefanya kazi kubwa katika kuwaandaa mabalozi ambao ni wawakilishi muhimu kimataifa. Lakini pia tumekuwa na kozi fupi za kuwaandaa wafanyabiashara za kimataifa pamoja na kuonyesha fursa zilizopo kwa wawekezaji wa kigeni hapa nchini," alieleza.

Aidha, amesema kuwa chuo kimetengeneza programu mpya zinazojielekeza katika ujenzi wa uchumi wilayani na mikoani ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa ndani na hivyo kufikiwa kwa azma ya uchumi wa viwanda.

Msajili wa Chuo, Dk. Ally Masabo, alitoa wito kwa Watanzania kujiunga na chuo hicho hasa katika kipindi hiki ambacho diplomasia ya uchumi imekuwa dhana muhimu katika kujenga uchumi za mataifa mbalimbali.

Chuo cha Diplomasia kilianzishwa mwaka 1978 na kinaendeshwa kwa ubia baina ya serikali ya Tanzania na Msumbiji kwa lengo la kutoa mafunzo ya diplomasia, stratejia pamoja na lugha.

# NHC yapunguza bei ya viwanja mradi wa Arusha

**Na Munir Shemweta,** ARUSHA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limebadilisha viwango vya bei za kuuzia viwanja vyake kwenye mradi wa Safari City mkoani Arusha kwa kutoa punguzo la asilimia 40 kwa viwanja vyote.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa NHC mkoa wa Arusha, Ladislaus Bamanyisa, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa Safari City kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, alipotembelea mradi huo akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya NHC pamoja na uendaji kazi wa sekta ya ardhi katika mkoa wa Arusha.

Bamanyisa alisema uamuzi wa kubadilisha viwango vya bei za mauzo katika mradi huo kumesababishwa na kusuasua kwa mauzo ya viwanja katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019, ambapo shirika limeuza viwanja sita tu kwa kile alichokieleza hali ngumu ya kiuchumi.

Kwa mujibu wa meneja huyo, viwango vipya vilivyopitishwa ni vile vya makazi ambapo sasa itakuwa Sh. 21,000 kwa kila mita ya mraba badala ya Sh. 35,000 na Sh. 27,000 badala ya Sh. 45,000 kwa viwanja vya biashara.

Aliongeza kuwa tangu kuzinduliwa mradi wa Safari City Juni 2016, Shirika limeuza jumla ya viwanja 589 vyenye thamani ya shilingi 13,097,198,200 na kukusanya shilingi 7,981,887,540 sawa na asilimia 61 ya makusanyo kwa viwanja vilivyouzwa.

Hata hivyo, alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 NHC imeuza viwanja 122 vyenye thamani ya Sh. 2,058,113,600 na kukusanya Sh. 453,952,600 na kubainisha kuwa viwanja vilivyobaki na kuendelea kuuzwa ni 1,252.

Kwa upande wake Mabula ameitaka NHC kuongeza kasi katika kukamilisha mradi wa Safari City kwa kuweka miundombinu ili kupata mafanikio kama ilivyo dhamira ya shirika.

Alisema, shirika linatakiwa kuhakikisha eneo la mradi linakuwa na miundombinu imara kama barabara, maji pamoja na umeme ili kuwavutia wateja wanaotaka kununua viwanja vya mradi.

"NHC inatakiwa kushughulikia miundombinu hapa, adha anayoipata mteja anayenunua kiwanja na kufika eneo lake ni ngumu na hasa mvua ikinyesha atafikaje? Inabidi ajifikirie mara mbili kununua eneo hilo," alisema Mabula.

Kwa mujibu wa Mabula, ukosefu wa miundombinu inachangia eneo la mradi wa Safari City kutopata wateja na kubainisha kuwa mawasiliano na watoa huduma yawe karibu ili mji uweze kupendeza.

Aidha, Mabula ameitaka NHC kuhakikisha pia inautangaza mradi wa Safari City kupitia vipindi vya televisheni na radio ili kuwawezesha wananchi kuutambua na kununua viwanja vya mradi huo na hivyo kuingizia shirika mapato.

Pia aliitaka NHC kufikiria utaratibu wa kuwakopesha watumishi wa umma viwanja vya mradi huo kwa njia ya kulipa kwa awamu tofauti na ilivyo sasa, ambapo shirika limekuwa likiwafikiria zaidi wafanyabiashara.

Mradi wa Safari City wenye eneo la ukubwa wa ekari 587.03 lenye viwanja zaidi ya 2,141 ulianzishwa na NHC ili kusaidia uendelezaji na usimamizi madhubuti wa mpango kabambe wa jiji la Arusha kama ulivyoandaliwa, kusaidia kupunguza uhamiaji holela pamoja na kuwawezesha watu binafsi, kampuni na taasisi mbalimbali kupata maeneo yenye huduma muhimu za kijamii.

# Wauguzi, madaktari wasaidiwa vifaa vya kujikinga na corona

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Oxfam limekabidhi vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa virusi vya homa kali ya mapafu (Covid-19) kwa wauguzi na madaktari wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, vyenye thamani ya shilingi milioni 29.8 kwenye vituo vinne vya afya.

Vituo hivyo vya afya ni Lunguya, Chela, Nganya na Kituo cha Afya Bugalama ambapo vituo hivyo vinahudumia wagonjwa wengi sana ukilinganisha na zahanati zilizopo kwenye halmashauri hiyo.

Akikabidhi vifaa hivyo jana Mratibu wa Shirika hilo Kanda ya Ziwa, Valentine Shibula kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Simon Berege, alisema kuwa, lengo la kutoa vifaa hivyo ni kuwakinga na maambukizi wauguzi na madaktari wanapokwa wanawahudumia wagonjwa katika vituo vya afya maalum vilivyotengwa na serikali.

Aidha, Shibula alitaja vifaa vilivyotolewa kuwa ni barakoa za (N95) 240, mavazi maalum ya kujikinga na corona (PPE), jezi 60, vidonge vya kutakasa vifaa tiba vinavyotumika kwa wagonjwa kopo 12 na barakoa za kawaida pakiti 978 ambavyo vyote vimegharimu kiasi cha shilingi milioni 29.8.

Akipokea vifaa hivyo, Berege alilipongeza Oxfam kwa kuiunga mkono serikali katika mapambano dhidi ya covid-19 na kuahidi kuwa vitatumika ilivyoelekezwa katika kituo maalumu cha uangalizi wahisiwa wa corona cha Bugarama.

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Ernest Chacha, alisema wanaendelea kutoa elimu ya kujikinga na Covid-19 kwa wananchi hususani katika maeneo yenye mikusanyiko.



Mratibu wa Shirika lisilo la kiserikali la Oxfam, Kanda ya Ziwa, Valentine Shibula (kulia), akimkabidhi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Simon Berege, mavazi maalumu ya kujikinga na Covid-19 (PPE) yenye thamani ya Sh. milioni 3.6 kwa ajili ya wauguzi na madaktari wa vituo vya afya vya halmashauri hiyo, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**.

# Wazazi wahimizwa kuwalinda watoto maambukizi ya corona

**Na Futuna Seleman,** RUFIJI

WAZAZI wilayani Rufiji mkoani Pwani katika kipindi hiki cha corona wametakiwa kuhakikisha mtoto anabaki nyumbani na kuandaliwa michezo ya kuwachangamsha katika mazingira salama.

Aidha, wazazi ama walezi wametakiwa kufuatilia mienendo ya watoto wao ili kuwakinga na ubakaji, ulawati na mimba kwa kuwa mtoto anaweza kufanyiwa vitendo hivyo na kukaa kimywa bila kutoa taarifa.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Rufiji, Hussein Akhmed, aliyasema hayo katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika wilayani humo.

"Mzazi au mlezi hakikisha kuwa mtoto hafanyi kazi hatarishi mfano migodini, viwandani, mashamba makubwa na uvuvi hiyo ni kesi jinai kumtumikisha mtoto katika maeneo hayo... pia ni kinyume cha sheria mtoto kuwa kwenye baa, kumbi za starehe na vilabu vya pombe hasa nyakati za usiku," alisema.

Baadhi ya wazazi walezi wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti juu ya ulinzi wa mtoto, walisema jukumu la malezi ya watoto ni la msingi katika kipindi hiki cha ugonjwa wa corona.

Alisema jamii haipaswi kuwaacha watoto wakihangaika wakati wa likizo ya corona kwa kuwa kufanya hivyo ni kuwatafutia watoto matatizo ikiwamo kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

"Mtoto ana haki ya kucheza, kusikilizwa na kulindwa, hivyo ni jukumu letu wazazi kuwafuatilia hata kama shule zilifunguliwa," alisema Athman Mketo, mkazi wa Chemchem Rufiji.

Naye MKuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njwayo, aliwataka wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao na kuwatunza kuhakikisha wanachukua hatua za kupambana na maambukizi ya corona wakati wa kipindi hiki cha likizo ya dharura wakiwa nyumbani na baada ya shule kufinguliwa.

Alisisitiza kuwa jukumu la kulea watoto ni jukumu la mzazi, mlezi na jamii kwa ujumla kuhakikisha haki zote anazostahili mtoto anazipata.

## Viongozi wa dini wataka kampeni za kistaarabu

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

KAMATI ya Amani Mkoa wa Mwanza, imevitaka vyama vya siasa, wanasiasa nchini hususani wagombea, kuacha kufanya siasa za fitina, ubaguzi, pamoja na uvunjifu wa amani katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana jijini Mwanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya viongozi wa dini mkoani hapa, Shehe Hassan Kabeke, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, akitaka kuwapo na siasa za amani, 2020.

"Vyama vya siasa nchini, wanasiasa hususani wagombea wanatakiwa kuzingatia miiko katika kampeni zao kuelekea uchaguzi mkuu mwaka huu, wasitumie lugha za matusi jukwaani, kuchafuana, vurugu pamoja na kuleta uvunjifu wa amani," alisema Kabeke.

Alisema viongozi wa dini hawatafurahishwa kuona wagombea wakifanya siasa za fitina, uvunjifu wa amani na kwamba siasa za aina hiyo hazikubaliki kwa viongozi wa dini.

## Jumuiya za CCM zaonywa ubaguzi

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

JUMUIYA za Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani zimetakiwa kutobaguana katika kipindi hiki cha uchaguzi na badala yake kuungana na kushirikiana ili kumaliza vizuri uchaguzi mkuu.

Rai hiyo imetolewa juzi mjini Kibaha na mlezi wa CCM Mkoa wa Pwani, Gaudensia Kabaka, wakati akizungumza na baadhi ya wanachama katika ofisi za CCM Mkoa zilizopo Mjini Kibaha.

"Tukubaliane katika hili tusibaguane, jumuiya zote ni wamoja kwa kufanya hivyo tutafanikisha kupata viongozi bora kutoka kwenye chama chetu ambao wanakubaliwa na wananchi," alisema.

Alisema ni zamu ya Mkoa wa Pwani sasa kushika namba moja kwa wingi wa kura za kumchagua rais, wabunge na madiwani katika uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba.

Kwa upande wake Katibu wa CCM mkoa wa Pwani, Makoa Ally, alisema chama hicho kitazingatia maelekezo yaliyotolewa na mlezi huyo.

"Tunaahidi tutazingatia tulichoelekezwa na mlezi wetu ni kuona tunaongoza kwenye kura tumejipanga kwa hilo na tunamwambia hatutamuangusha," alisema Makoa.

Kabaka ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT) Taifa, amechukua nafasi ya ulezi wa Mkoa wa Pwani kutoka kwa Samia Suluhu Hassan.

# Hasunga: Kuna ziada ya chakula

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imesema pamoja na kuendelea kuwapo kwa ugonjwa wa homa ya mapafu (Covid-19) katika baadhi ya nchi mbalimbali, lakini uzalishaji wa chakula nchini umeendelea kuimarika na kujitosheleza kwa asilimia 100.

Aidha, imesema kuna ziada ya takribani tani milioni 2.8 ambazo huuzwa nje ya nchi hususani kwa nchi jirani na Tanzania.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Kilimo, Japhet Husunga, wakati akizindua maonyesho ya kilimo biashara yaliyofanyika katika Kijiji cha Majambaa Kata ya Msowero, wilayani Kilosa, mkoani Morogoro yaliyoambatana na wakulima katika wilaya hiyo kuonyeshwa mashamba darasa ya mazao mbalimbali yalivyoongeza tija kutokana na mbegu za teknolojia za kisasa zilizofanyiwa utafiti.

Waziri Hausunga alisema kuwa kuwapo kwa ziada ya chakula ni jambo la kujivunia na kuendelea kumshukuru Mungu kwa kuwa baadhi ya nchi ikiwamo majirani zinakabiliwa na upungufu wa chakula kufuatia kuendelea kuwapo kwa ugonjwa huo.

Hata hivyo, alisema pamoja na mafanikio hayo, bado kilimo kina changamoto mbalimbali zikiwamo matumizi hafifu ya pembejeo kama matumizi ya mbegu bora, mbolea, viuatilifu, mabadiliko ya tabianchi ambayo husababisha kuibuka kwa aina mpya ya visumbufu vya mazao na upungufu wa rutuba ya udongo na upotevu wa mazao baada ya mavuno, masoko na ukosefu wa mitaji kwa wakulima walio wengi.

Alisema serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali kupitia Taasisi ya Utafiti Tanzania (TARI) kufanya tafiti kwa ajili ya kutatua changamoto hizo zilizoanza sasa kuongeza tija za uzalishaji, uhamasishaji wa matumizi ya pembejeo, kutoa elimu kupitia mashamba darasa, kuhaulisha teknolojia rafiki kwa kuzingatia uzalishaji na usindikaji mazao kwenye mnyororo wa thamani.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti cha Tari Ilonga, ambacho ndicho kimeandaa maonyesho hayo, Dk. Joel Meliyo, alisema wameamua kuzipeleka teknolojia za mbegu za kisasa walizozifanyia utafiti na kuleta tija moja kwa moja kwa wakulima kupitia mashamba darasa katika kila kata za Wilaya ya Kilosa ili wakulima waweze kubadilisha kilimo kuwa cha kibiashara.

"Tumekuwa tukifanya utafiti mbalimbali wa mbegu za teknolojia ya kisasa na kukaa nazo pale ofisini, sasa tumeamua kuwaonyesha wakulima kwenye mashamba darasa katika maeneo yao," alisema na kuongeza:

"Tunataka waondokane na kilimo cha mazoea na kulima kilimo cha kisasa chenye tija na ziada kufanyia biashara."

Alisema kuwa maonyesho hayo yatakuwa yakifanyika kwa kipindi cha mwaka mzima kwa kuonyesha na kufundisha wakulima matumizi ya teknolojia hizo.

Mmoja wa wakulima kutoka Kijiji cha Majambaa, Shukuru Mwaibale, alisema kupitia shamba hilo darasa ameweza kuachana na kilimo cha mazoea cha kutumia mbegu za asili na kulima kwa kutumia mbegu hizo za teknolojia ya kisasa ambazo anatarajia kuvuna gunia kati ya 25 mpaka 30 kwa ekari moja wakati kabla ya hapo alikuwa akivuna gunia nane mpaka 10.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema ameshatoa maelekezo kwa wakurugenzi wa vituo vyote 17 vya TARI kwa ajili ya kufanya maonyesho hayo kwa kuwafuata wakulima katika maeneo yao na kuanzisha mashamba darasa ili kuwafundisha teknolojia za kisasa.




Meneja wa Kitengo cha Biashara cha Kampuni ya Bima ya Sanlam Life Insurance, Mary Mtega (kulia), akimkabidhi Ofisa wa Benki ya NMB Tawi la Clock Tower Arusha, Edu John, makabrasha ya bima ya elimu, baada ya kutoa mafunzo kwa maofisa wa benki hiyo, jijini Arusha juzi. **PICHA: GIFT THADEY**.

# Taasisi zasaidia shule, vyuo vita ya corona

**Na Futuma Seleman**

TAASISI ya Dorice Mollel inayosaidia jamii na watoto waliozaliwa kabla ya wakati kwa kushirikiana na Taasisi inayosaidia jamii katika sekta ya elimu, afya TIKA ya Uturuki zimetoa misaada mbalimbali ya vifaa vya kujikinga na corona kwa vyuo na shule za sekondari.

Baadhi ya vifaa hivyo ni katoni zaidi ya 3,000 kwa shule za sekondari na vyuo Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Mwanzilishi wa Taasisi hiyo, Dorice Mollel, alikabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Sophia Mjema ofisini kwake jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo, alisema ni katika kuunga mkono jitihada za Rais John Magufuli katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona.


"Mimi kama mwanzilishi wa taasisi hii nimeona pia 'modified' kundi hili la vijana wenzangu katika mapambano ya ugonjwa wa corona ingawa pia nasaidia sana kundi la watoto wanaozaliwa kabla ya wakati wao kama mimi kwa kutoa misaada hospitalini kwenye wodi za wazazi na watoto, pia jamii yenye mahitaji maalum," alisema Dorice.

Aliihimiza jamii kutobweteka katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona kwa kuchukua tahadhari zote kama miongozo ya Wizara ya Afya inavyoelekeza.

Kwa upande wake DC Mjema akipokea msaada huo alisema utasaidia mapambano dhidi ya corona.

"Tunathamini na kutambua mchango unaotolewa na Taasisi ya Dorice Mollel na pia TIKA ya Uturuki nchini, tunaomba na wadau wengine wajitokeze kuchangia vifaa vya kujikinga na corona ili kuutokomeza ugonjwa huo," alisema Mjema.

Aliongeza kuwa mapambano dhidi ya corona yanapaswa kuungwa mkono na jamii yote kwa ujumla hasa ushiriki wa wadau wa maendeleo katika kuendelea kutoa elimu kwa jamii na misaada mbalimbali ikiwamo sabuni za kuoshea mikono," alisema.




Ukurasa 13

Hospitali hii ipewe jina Mama Maria Nyerere - 1



Ukurasa 12

**Shubiri ya ufundi duni, umaskini vinautumbukiza shimoni mradi**

BUFE

IJUMAA JUNI 19, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Subira Mgalu sambamba na miradi ya kinamama Pwani

## • Wenye ulemavu sehemu ya mbeleko



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Walemavu, Stella Ikupa, alipokabidhi vyerehani kwa kundi la watu wenye ylemavu vilivyotolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu. **PICHA: JULIETH MKIRERI.**

**Na Julieth Mkireri, Kibaha**

"TULIUMIZA vichwa kwa muda mrefu nini tufanye kama mradi wetu wa kuwakwamua kiuchumi wanawake kuanzia ngazi za kata hadi mkoa, katika Jumuiya ya Wanawake (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi hatimaye leo tumepata mkombozi."

Ni maneno yaliyotolewa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Pwani, Farida Mgomi, akimnyooshea kidole aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu Pwani na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alipompongeza kutumia vizuri nafasi yake.

Farida alisema, Jumuiya hiyo imekuwa ikijitafakari miradi ya kuanzisha, kumuondolea mwanamke utegemezi kwenye familia, kitendawili kilichotenguliwa na aliyekuwa mwakilishi wao bungeni, Subira Mgalu.

"Jumuiya zetu sasa zitatumia vyerehani walivyopatiwa na Mgalu kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya ushonaji, pia itasaidia kutengeneza ajira kwa vijana ambao walikuwa majumbani hawana kazi" anasema Farida.

Mwenyekiti wa UWT Wilaya Kibaha Mjini, Judith Mruge, alifafanua kwamba vyerehani alivyotoa Subira mkoani Pwani, vitasaidia kuwapatia shughuli za kujiinua kiuchumi na kuwa na maendeleo.

Aliwasihi wanawake kushikamana na kuwa mbali na utengano, huku wakiwapa nafasi wanaowaamini wana uwezo kuwaongoza na kutumia nafasi zao katika harakati za maendeleo.

Judith alisisitiza wanawake wapendane na washikamane kwa mazuri, kwani vita vina kawaida ya kudidimiza safari ya kuelekea kwenye maendeleo.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Mkoa wa Pwani, Tatu Kondo, anampongeza Subira kwa kutolibagua kundi hilo, kwani amekuwa akiwatembelea na kuwapatia vitendea kazi.

Watu wenye ulemavu walipatiwa jumla ya vyerehani 29, ambavyo wilaya zote za mkoa wa Pwani zimenufaika, huku katika ofisi ya Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu, nao watapatiwa kuendeleza mradi wa ushonaji, ulotembelewa na mgeni Subira hivi karibuni.

Tatu aliahidi, vyerehani hivyo vitatumika kuwainua kiuchumi na kuwaondoa katika hali ya utegemezi.

Diwani mwenye ulemavu wa ngozi, anayejitambulisha kwa jina la moja la Thomas, alimpongeza Subira kwa kulikumbuka kundi hilo, naye akimuahidi vyerehani hivyo vitatunzwa vidumu kwa muda mrefu na kuwaletea mabadiliko ya kiuchumi wengi.

Alisema, amekuwa akifanya kazi ya kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi, kwani wengi wanaoaminiwa wamekuwa viongozi wazuri kwenye jamii, katika uwezo unaofanana na wanaume.

**MWENZAKE AMPONGEZA**

Pia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Walemavu, Stella Ikupa, naye aliungana kumpongeza Subira kwa kuwakumbuka walemavu na kuwasaidia vitendea kazi.

"Ungetoa vyerehani kwa Jumuiya ya UWT pekee tungesema uko kwenye kampeni, lakini hawa watu wenye ulemavu, hizo kura watakupigia wapi? Nakupongeza kwa hili," alitamka.

Stella alisisitiza umuhimu wa kuwapo wakalimani kwenye mikutano ya kampeni zijazo, ili watu wenye ulemavu wa wasikie na kuelewe sera za wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi .

**MWENYEWE AFUNGUKA**

Subira alisema ametoa jumla ya vyerehani 400, ambavyo vinagawiwa katika kata zote za mkoa wa Pwani, ili jumuiya na kundi la wenye ulemavu waanzishe miradi ya ushonaji na kujiingizia kipato.

Alitamka kutambua changamoto za watu wenye ulemavu baada ya kuwatembelea na aliamua kuwapelekea msaada huo, ili uwasaidie kufungua mradi wa ushonaji kwa kila wilaya.

Kiongozi huyo alisema, katika msaada wake huo angelipa kodi ya pango kwa miezi sita kila wilaya, eneo ambalo mradi wa ushonaji utafanyika, kwa kinamama na watu wenye ulemavu.

"Pia, niko tayari kuwadhamini masomo vijana wenye ulemavu ambao wana sifa za kujiunga na vyuo vya ufundi," alisema Subira.

"Tutumie vyuo vya ufundi kusomesha watoto wetu si jambo dogo tukidhamiria linaweza kututoa hatua moja hadi nyingine na kuanzisha viwanda vidogo vidogo," alisisitiza.

Kuhusu UWT, Subira alishauri vyerehani aliyogawa vitumike kuzalisha ajira zitakazowainua kiuchumi kinamama kwa ujumla, huku akifafanua amewekeza kiasi kikubwa katika kusaidia sekta za afya na elimu.

UCHUMI

NISHATI GESI YA SAMADI

# Shubiri ya ufundi duni, umaskini vinautumbukiza shimoni mradi

## • DC Muro awafuatilia wafadhili warudi

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa Arumeru**

***IJUMAA iliyopita ilikuwa sehemu ya kwanza ya makala hii kuhusu mradi wa nishati ya gesi wilayani Arumeru na namna inavyoleta ahueni ya kiuchumi dhidi ya dhiki ya kuni. Endelea na safu ya pili.***

"HUU mtambo wa baiogesi uliharibika wenyewe, gesi ilikuwa haitoki. Nilimjulisha fundi, alivyokuja akanimbia nikitoe kinyesi hapa. Najiuliza hiki kinyesi nakitoa vipi katika huu mtambo?" Ni maneno ya Unice Palanjo, aliyekuwa akihaha kupata suluhu ya kutengenezewa mtambo wake.

Anasimulia kuwa nishati hiyo kabla ya kuharibika, ilikuwa ikimsaidia kupunguza matumizi ya kutafuta kuni, hivyo kwa sasa imegeuka shubiri baada ya kukosekana ufundi.

Palanjo, mkazi wa kijiji cha Oldonyowas wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, anaeleza kukosa matumaini ya kuendelea na nishati hiyo mbadala itokanayo na kinyesi cha ng'ombe.

Arusha inaongoza kuwa na wafugaji 111,183 sawa na asilimia 45 nchini kwa mujibu wa takwimu za Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2016, huku ikiatajwa kuwa kinara wa kutumia kuni, kwa wastani wa kaya sita kati ya 10 zinatumia kuni kupikia.

Hiyo ni kwa mujibu wa Ripoti ya Upatikanaji Nishati Tanzania Bara, kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), mwaka 2016 na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Wananchi wa kijiji hicho walihamasishwa kutumia nishati mbadala ya kinyesi cha ng'ombe kupika chakula, lengo ni kupunguza matumizi ya kuni na kutunza mazingira.

Ilipoanzishwa, wananchi hao walichangamkia fursa hiyo na kupatiwa mtambo wa baiogesi waliofungiwa kwa gharama ya Sh. 215,000 pamoja na jiko la kupikia.

### CHANGAMOTO

Ingawa kuna wengi walioshangilia kuibuliwa kwake wapo waliobaki katika machungu, sababu ni kushindwa kuitumia, hususan wanapokumbwa na gharama za kukarabati miundombinu.

Ni hali inayoendana na shaka ya watumiaji hao, baadhi wakihoji ukweli wa tetesi zinazodai wenye mradi wamerudi kwao nchini.



Mkulima wilayani Arumeru, akiwa kwenye chanzo cha nishati ya gesi ya samadi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **Anaendelea kwa kuhoji: "Hivi unawezaje kuzoa hiki kinyesi? Hapo ndipo paliponishinda na ndio maana nimeshindwa kuendelea na mtambo huo, maana huu ni mtihani juu ya mtihani, mafundi wenyewe hawawezi wanakuja kutuambia sisi tutoe kinyesi chote."**

Palanjo anataka adha ya fundi, pale anapomuita afike mtengenezaji huyo, anaanza kwa kutoa kinyesi chote katika mtambo, jambo analodai ni mtihani kwao wamiliki.

Anaendelea kwa kuhoji: "Hivi unawezaje kuzoa hiki kinyesi? Hapo ndipo paliponishinda na ndio maana nimeshindwa kuendelea na mtambo huo, maana huu ni mtihani juu ya mtihani, mafundi wenyewe hawawezi wanakuja kutuambia sisi tutoe kinyesi chote."

Pia, kuna wanaolalamikia gharama za ufundi wa mitambo hiyo ya baiogesi, pindi inapopata tatizo kubwa na mwenyeji, Neema Lucas akiwa na ufafanuzi wa kiufundi kwamba, kuna wakati mipira iliyowekwa inasababisha gesi kupotea njiani, hata kumlazimu kumuita fundi.

Kwa mujibu wa Neema, hapo ni gharama inayoanzia Sh. 20,000 kutegemea na tatizo na ana ufafanuzi: "Sisi anatujua hivyo wakati mwingine tunamuomba tunamlipa Sh. 10,000 ingawa hii hela ni kubwa kulingana na maisha yetu hapa kijijini."



Viongozi wakijifunza jambo kuhusiana na umeme unaotokana na kinyesi cha wanyama.

Obed Mollel, mkazi wa kitongoji cha Zahanati, anarejea kilichopo kwa wanufaika wa awamu ya kwanza ya mtambo, kwamba iliharibika na hawajarekebishiwa.

Anasema ni hali inayowapa hofu pale mtambo utakapoharibika, kwani hawajui watakapopata msaada, kwa sababu kuna changamoto zilizojitokeza awali bado hazijashughulikiwa.

Mollel anasema alipojiunga na mradi wa baiogesi, aliahidiwa nishati hiyo ingekuwa na uwezo wa kuwasha taa, jambo ambalo halijatekelezwa, ikiishia kuwasha kupikia pekee na hadi sasa hawana mawasiliano na mwekezaji, aliyeondoka kurudi kwao, Italia.

### URIO ASEMA

Wakati wananchi wakilalamika suala la kuharibika kwa miundombinu ya Biogas bila kupata msaada na mitambo hiyo kuiacha, Ombeni Urio, mwenye kampuni iliypjenga mitambo ya Oikos na kuna wakati ardhi inachangia kupotea kwa gesi.

"Ukiona mpaka unaambiwa uzoe kinyesi katika mtambo, ina maana tumefanya jitihada zote za kutafuta 'likeji' ikashindikana ndio maana tunamuambia akitoe kinyesi ili tujue tatizo lipo wapi," anasema.

Urio anafafanua urefu wa kuchimba mtambo ni mita 1.85 sawa na mita sita za ujazo, zinajazwa lita 6,350 za kinyesi mmiminiko.

Anasema mteja anaposhindwa kutoa kinyesi katika mtambo huo, mbadala wake anatakiwa kugharamia Sh.180, 000 iwapo wameufunga wao na kama ni kutoka kampuni nyingine Sh 400,000.

Urio anasema, jiografia ya udongo wanayojenga mitambo ya nishati mbadala, kuna wakati ardhi ya eneo inadidimia bila wao kujua na anaongeza: "Kuna maeneo ardhi hudidimia na wahusika wa eneo hawana uelewa na ardhi yao.

"Sasa tunapoweka mtambo ardhi ikididimia na ule uzito wa kinyesi ambao unawekwa mtambo unaweza kugeuka na kusababisha gesi kutawanyika na kuanza kutokea pembeni kwa mtu kama huyu ni lazima atoe kinyesi chote ili asaidiwe tatizo lake."

### SHIDA KUJITAKIA

Kasoro zingine Urio anazieleza: "Wakati mwingine ni uzembe wao kutokulisha kwa wakati yaani anapunguza ng'ombe au kutokulisha kwa wakati. Hii nayo ni changamoto itakayomfanya asipate gesi wakati anapotaka kupika.

"Kuna wengine imetokea 'leakage' (uvujaji) kwenye pampu tunaenda kumrekebishia, watu wanalima bila kuangalia kama paipu imepita na kutoboa bila kujua. Inabidi tumbadilishie, kwani hujikuta gesi inashuka kila wakati," anafafanua Urio.

Kuhusu dai la gharama kubwa wanazotozwa watumiaji umeme wa gesi, Urio anasema inaendana na ukubwa wa tatizo ulivyo, akidai ni kati ya Sh. 10,000 hadi Sh. 50,000.

Anasema, kuna wanaojaza maji mengi katima gesi ambayo kiufundi ni kosa, kwa sababu wadudu anaowataja kwa jina la anarobian' hutengeneza gesi wanaposhambulia mlo na wanapokosa chakula ambacho ni kinyesi cha ng'ombe, gesi haiwezi kutengenezwa.

### DC MURO

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, anasema walikuwa katika subira ya nyendo za ugonjwa wa virusi vya corona umalizike, ili wafadhili hao wafanye mapito ya mradi wao.

"Zipo baadhi ya familia zimeshindwa kutumia mradi huo. Sisi tulichofanya ni kuwaomba wenzetu wa Oikos kutengeneza mradi wa pili ya mapito ya mradi, ili tuone tunaweza kufanya nini ya kuhakikisha tunawasaidia hawa wananchi ambao wamekumbwa na changamoto," anasema Muro.

Anaendele:"Mimi nikiwa kama kiongozi Mkuu wa Wilaya, siwezi kulalamika kwamba wananchi wangu hawakuwa na uelewa na jukumu letu ni kutatua changamoto."

.Muro anasema, namna ya kutatua changamoto hiyo ni kuomba marejeo ya mradi, waweze kufanikiwa na muhimu wenzao wa kampuni ya Oilcos iwatafutie fedha zitakazosaidia kuwaleta wataalamu.

Anasema mradi huo makao makuu yake yako nchini Italia, ambako kuliathirika sana na ugonjwa huo hata kukwamisha mradi.

"Wengi wapo Italia baada ya shughuli hizi kukamilika. Walifunga ofisi na kurudi kwao, hawakujua kama janga lingekuwa kubwa kiasi hiki," anaeleza


Anasema katika namna ya kupata suluhishi ya dharura hiyo, alizungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Arumeru, awatumie wataalamu waliokuwepo kuwasaidia.

Katika hilo, Muro anatoa rai kwa wananchi wenye changamoto yoyote ya nishati uhakikisha wanatoa taarifa kwa viongozi wao, akieleza: "Ombi langu wapitie ngazi husika kwa maofisa watendaji wetu wa kata ili taarifa zao ziweze kuja kwetu ili tuweze kuwasaidia."

Muro anakiri kuwa bado hana takwimu halisi ya wanaokabiliwa na changamoto katika mradi huo wa baiogesi, kwa sababu wanajitokeza mmoja mmoja mmoja.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hospitali hii ipewe jina Mama Maria Nyerere - 1






**NA JOSEPH KULANGWA**

MWALIMU wangu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Euphrase Kezilahabi (marehemu) alinifundisha, kwamba kila kitu duniani kina pande mbili; kina chanya na hasi, kina kulia na kushoto, pia kina juu na chini.

Alisema kila kitu kina upinzani wake na katika upinzani huo, huzaliwa kitu kingine ama chenye manufaa au kisicho na manufaa. Lakini yote hayo yanategemea na mnufaika wa pande hizo na kinachozaliwa kutokana na matokeo hayo.

Kumbe ndiyo sababu katika nishati, hasi na chanya huzaa umeme na katika viumbe, -ke na -me huzaa mtoto. Chanya haiwezi kutengeneza umeme bila kukutanishwa na hasi, hali kadhalika mwanamke hawezi kuzaa mtoto bila kukutana na mwanamume.

Ndivyo alivyojifunza Profesa Kezilahabi, ili naye aje atufundishe sisi, kwa kuwa elimu ni mchakato wa kuhamisha maarifa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Nami nilipata maarifa hayo kutoka kwa msomi huyo galacha, Mungu aendelee kuiweka roho yake peponi.

Wakati Profesa Kezilahabi anayafanya hayo kwangu, kijana (wakati huo), John Joseph Magufuli, naye alikuwa darasa lingine chuoni hapo akijifunza Hesabu na Kemia.

Leo ni Rais, Dk. Magufuli. Ni Rais wa Tanzania, ambaye hakutarajiwa na wengi kuitwaa nafasi hiyo, lakini ni Rais ambaye leo amefanya makubwa katika miaka yake hii mitano.

Ndiyo, Mungu akijaalia pengine atakuwa katika miaka yake mingine mitano na ya mwisho na inshallah, atafanya makubwa zaidi ya kumsaidia Mtanzania na pengine kuwa mfano wa kuigwa katika uongozi. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni.

Nasisitiza, ni mengi ameyafanya na siwezi kuyaorodhesha yote, lakini mimi kwa sababu maalumu, nitataja machache hasa yanayomgusa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere (marehemu) moja kwa moja.

Rais Dk. Magufuli amejitahidi kwa uwezo wake na kiwango chake kufufua na kukamilisha njozi za Mwalimu Nyerere katika masuala mbalimbali, hususani ya ujenzi wa miundombinu.

Anajenga chanzo kikubwa cha nishati ya umeme katika Mto Rufiji, kikijulikana tangu enzi za Nyerere, kama Stiegler's Gorge na sasa Mwalimu Julius Nyerere.

Ametekeleza kwa vitendo azma ya miaka mingi ya Mwalimu Nyerere ya makao makuu ya nchi na serikali kuhamia Dodoma, serikali iko Mtumba, Dodoma, Ikulu iko Chamwino, Dodoma.

Ni azma ya tangu miaka ya sabini, ikumbukwe ni miaka ambayo Tanzania bila kupenda iliingia katika vita vya Uganda, kwa ukubwa na uzito wa vita vile kiuchumi, isingewezekana tena kuingia gharama ya kuhamia Dodoma wakati huo.

Hata awamu zilizofuata baada ya ile ya kwanza, hazikuweza kuitekeleza kutokana na mizigo mingine ya ujenzi wa uchumi, hivyo kukosekana uharaka wa kuhamia Dodoma, ambazo uamuzi wake ulitokana na mkoa huo kuwa katikati ya nchi, hivyo kurahisisha mawasiliano ya walio mikoani kufika makao makuu.

Kuanza kwa matumizi ya teknolojia ya mawasiliano, nako kulibwetesha akili za Watanzania na kukosekana msukumo na ari ya kuharakisha kuhamia Dodoma na baada ya mambo kuelekea kukaa sawa kiuchumi, hivi sasa ikawa rahisi kwa Dk. Magufuli kusimamia na kutekelezwa bila sababu yoyote ya kuzuia.

Watanzania wameanza kuizoea Dodoma kama Wanigeria walivyoizoea Abuja, baada ya kuhama kutoka Lagos. Ni jambo la kupongeza, kwamba ndoto ya Nyerere hatimaye imetimia, kama ambavyo itakuja kutimia ya umeme wa Mto Rufiji.

Ni dhahiri sasa, kwamba Hesabu na Kemia alizojifunza Mlimani, ndivyo vimempa mwanga wa kuona kwamba kumbe unaweza ukapanga na kuchagua na ikawezekana na sasa, Dodoma ni makao makuu ya Tanzania kivitendo na umeme mkubwa unatazamiwa kutoka Mto Rufiji. (Itaendelea)

**Simu: Simu: +255 713 410008 na barua pepe: jkulangwa@yahoo.com**

BIASHARA

# Corona inaifanya zao tangawizi iwe kimbilio masoko nje, ndani



Mandhari tofauti ya bidhaa tangawizi zikiwa sokoni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

KILIMO kitaanza kuwa cha kijani kwa hatua kutokana na hitaji la mboga na mazao mengine ya kuongeza vitamin mwilini, hasa Vitamin C inayosifika katika maeneo tofauti duniani.

Kuna nadharia za kinga dhidi ya uharibifu mwilini, endapo mtu anaambukizwa virusi vya corona. Ni ugunduzi unaotokana na jitihada za kutafuta dawa za asili katika maeneo mengi duniani, hasa Afrika na Asia.

Huko ni mahalo ambako kuna utamaduni uliodumu kwa karne kadhaa kabla ya Mapinduzi ya Viwanda barani duniani. Ni katika mandhari hayo, ambako aina tofauti za dawa ya Covid-19 zilijaribiwa.

Licha ya kuwapo michanganyiko tofauti hasa ya kuandaa mchemsho wa mazao au majani, yanayotumika kufukiza watu kuinua joto mwilini na kuzuia kushamiri wa virusi vya corona kuingia.

Ni mazao mawili yaliyosikika zaidi baada ya mwezi mmoja hivi; malimau kwa upande mmoja kama tunda na tangawizi kwa upande mwingine kama mboga, licha ya kuwa inatumika zaidi katika chai maeneo ya mijini.

Kuna mmea mwingine, mwarobaini, ambao sasa unatumika kufukiza watu, ukitumiwa peke yake au pamoja na majani au mboga, kulingana na uelewa wa maeneo tofauti.

Matumizi ya dawa za miti yalianza kufuatiliwa kwa karibu kuelekea mwisho wa Aprili baada ya China kuonekana imefaulu zaidi katika kuzuia kuenea kwa virusi vya corona, ikisema imetumia pia dawa za miti 'za Kichina.'

> **Kutokuwepo uasilia wa kutumia miti, majani au mboga kama dawa Ulaya, mara nyingi zinaonekana ubabaishaji. Hata hivyo, kuna kiwango fulani cha kutambua kuwa tangawizi inaweza kutoa msaada kujenga kinga za mwili.**

Ilitaka ianze kuzieneza duniani, lakini mtazamo ulichochea watafiti dawa na waganga wa jadi kuwa na fursa zaidi ya kuzungumzia dawa za asili au za miti kutibu au kuzuia makali ya virusi vya corona, kama alivyosema mwanzoni, Waziri wa Afya, Meandeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

### KUJIFUKIZA 'DILI'

Siku zilivyozidi kupita na hasa hadi kufika mwezi uliopita, ikaanza kudhihirika kuwa kufukizwa ni 'dili' katika mapambano dhidi ya corona, huku hospitali zikihangaika wagonjwa wa corona watibiwe vipi.

Kukosekana dawa halisi ya kutibu virusi hivyo, wengi walipewa dawa za 'hapa na pale' kutibu mafua makali au homa, kulitoa nafasi kwa hisia kuwa kinga za mwili ndiyo jambo muhimu.

Nchi kadhaa zilianza kuona wimbi la wakazi mijini, kwa mfano Singapore ambako kimsingi ni kama sehemu ya Malaysia, waliingia madukani kutafuta vidonge vya Vitamin C zaidi au vya 'multi-vitamin.'

### KUIBUK A TANGAWIZI

Hapo ikaanza shauku ya kutafuta vianzio vya asili vinavyoongeza kinga mwilini kwa jumla. Mtu anaweza kusema tangawizi ilishinda mbio hizo za zao maalum ambalo kila mtu anahitaji kufanya sehemu ya anachokula au kunywa, ili kujiweka vyema dhidi ya maambukizo.

Kutokuwepo uasilia wa kutumia miti, majani au mboga kama dawa Ulaya, mara nyingi zinaonekana ubabaishaji. Hata hivyo, kuna kiwango fulani cha kutambua kuwa tangawizi inaweza kutoa msaada kujenga kinga za mwili.

Hivyo, tangawizi inaonekana kujengeka zaidi katika masoko ya ndani na kama inauzwa kwa wingi zaidi nje, huwa hivuki mipaka ya mbali.

Nchi za Ulaya na Marekani, kama ilivyo kwa Shirika la Afya Duniani (WHO), wanangoja kwa hamu kuanza kufanyiwa majaribio chanzo ya corona, kuelekea mwisho wa mwaka huu.

Bado wachambuzi wanashangaa imekuwaje Afrika kwa sehemu kubwa kutoingia katika wimbi kubwa la maambukizo kama ilivyo Ulaya na Marekani, huku Amerika hali inatikisa kwa kasi.

Tangawizi na matumizi yake kijamii siyo geni, iwe ni masoko ya nyumban na nje, ila haijawahi kupata upekee wa soko, kuwa zao linalohitajika kama dawa kwa aliye hatarini kuupata ugonjwa fulani.

Hivyo, licha kuwa vitamini zinazopatikana katika maziwa na mboga, matunda, nyama, samaki na vyakula vya aina mbalimbali, tangawizi imeanza kuwa na nafasi ya peke yake kama bidhaa au chakula na kinywaji muhimu cha kujenga kinga za mwili.

Kwa muda wa wastani wa mwezi sasa, zao hilo limeanza kupungua katika masoko ya mitaani (magengeni) ambako kunabidi wapate bei ndogo, ili nao wasipandishe bei kwa walaji, kwani hakuna uwezekano wa kuuza vitu ghali magengeni, labda viwe tayari vimeharibika.

Bado hakuna uhakika kama mwelekeo mpya wa uhitaji wa zao tangawizi, kama sehemu muhimu ya mahitaji ya kila siku na hata corona inaondoka, uhitaji wa tangawizi una nafasi sokoni.

Mtu anaposikiliza kinachotokea, anagundua umuhimu wa kuendelea kuchukua tahadhari, kwani yako maeneo kama China na Marekani ambako baadhi ya miji au majimbo hayakuwa na maambukizo kwa wastani wa mwezi au zaidi, halafu yakaanza tena.

Ina maana kuna mvutano wa kihisia katika matumizi ya pesa ndogondogo na kuangalia vinywaji gani vya kutumia mitaani, vitu gani vya kununua magengeni ili kutayarisha vyakula na vinywaji nyumbani, kama hitaji la tangawizi litaendelea kama sasa au kuanza kupungua.

Ila endapo itatokea wimbi la maambukizo ya virusi vya corona kusikika tena, itabidi wanaorudia maisha ya kawaida kwa vyakula na vinywaji wajiangalie upya waweke mkazo katika kuchukua tahadhari. Tangawizi itakuwa kimbilio hapo.







# Wenye ulemavu kuhamasishwa kugombea ubunge

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) mkoani Dodoma, limetakiwa kuwahamasisha watu wenye ulemavu kugombea nafasi za ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu mwaka huu ili kupata uwakilishi kwenye ngazi za uamuzi.

Sambamba na hilo, viongozi wa vyama vya siasa wameombwa kuwateua wagombea wenye ulemavu wenye sifa ili kushiriki uchaguzi huo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Ofisa Uchaguzi Jimbo la Dodoma mjini, Albert Kasongi, alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa ushawishi na utetezi kwa viongozi wa vyama vya siasa pamoja na watu wenye ulemavu katika michakato ya uchaguzi huo uliofadhiliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Foundation for Civil Society (FCS).

Alisema shirikisho na viongozi wa vyama vya siasa wahakikishe wanatoa ushawishi kwa watu hao waliopo kwenye makundi maalum ili kujitokeza kugombea nafasi hizo.

Alisema viongozi wa vyama hivyo ndiyo wenye mchakato mzima wa awali katika kuteua wagombea ni vyema kuwapitisha watu wenye ulemavu wenye sifa za kuwa viongozi.

"Katika makundi haya kuna watu wenye sifa za kuwa viongozi, pia michakato ya uchaguzi iwaangalie ili kutoa fursa kwao kwa kuwa wana uwezo wa kuwatumikia wananchi, lakini kupata uwakilishi kwenye ngazi mbalimbali za maamuzi," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Mradi wa Elimu Jumuishi, Wilaya ya Dodoma na Bahi, Jane Mgidange, aliwashauri wazazi na walezi wenye watoto ambao wana ulemavu kuhakikisha wanawajengea misingi bora ya kielimu, ili wawe viongozi.

"Ni muhimu kuwajengea mazingira rafiki ili kupata elimu itakayowatengeneza kuwa viongozi Naye Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Lailah Ngozi, aliwataka watu wenye ulemavu kujitokeza kwenye mchakato wa kugombea nafasi hizo na kuachana na woga.

Katibu wa Shirikisho hilo mkoani humo, Justust Ng'wantalima, alisema makundi ya watu wenye ulemavu hayajumuishwi kwenye ngazi ya maamuzi hivyo kushindwa kuwasilisha maoni yao kwenye vyombo mbalimbali.

# Tani 147 minofu samaki zasafirishwa nje ya nchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isaac Kamwelwe, amesema hadi sasa tani 147 za minofu ya samaki zimesafirishwa nje ya nchi kupitia uwanja wa ndege wa kimataifa Mwanza.

Kufuatia soko hilo, kamati imeundwa itakayotafuta masoko ya bidhaa mbalimbali ikiwamo minofu ya samaki kutoka Ziwa Victoria.

Kauli hiyo aliitoa juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kikao kilichowahusisha Waziri wa Kilimo, Uvuvi na Mifugo, Mambo ya Nje, Fedha na Mipango pamoja na wakuu wa mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara.

Kamwelwe, alisema Tanzania ilianza usafirishaji wa minofu hiyo Mei 20, mwaka huu, kupitia uwanja huo hivyo kikao hicho kililenga kujadili namna ya kuongeza usafirishaji wa minofu hiyo.

"Hivi sasa uwanja huu umekuwa wa kimataifa ndege zinatua na kupaa moja kwa moja kwenda katika nchi za nje zikiwa na bidhaa mbalimbali," alisema.

Alisema kikao hicho kimelenga kutafuta kampuni zingine za ndege ambazo zitaweza kutua moja kwa moja Mwanza na kubeba minofu hiyo ambayo ipo mingi.

"Pamoja na kusafirisha minofu ya samaki, lakini tumejadili na bidhaa nyingine ikiwamo nyama, maparachichi pamoja na mboga ambazo zinahitajika nchi za nje lazima tusafirishe kutoka hapa nchini ili wakulima wetu pia wapate bei nzuri," alisema Kamwelwe.

Vile vile alisema, tayari wameshaongea na kampuni ya ndege ya Rwanda, ambayo ndege zake zitaanza kutua moja kwa moja na kubeba mizigo za bidhaa mbalimbali kwenda nchi nyingine.

"Uwanja huu zile changamoto zilizokuwapo kama za uzio tayari zimeshaanza kufanyiwa kazi, uzio umeshaanza kujengwa, mitambo ya kupakia minofu ya samaki tayari imeshafungwa hivyo yale malalamiko ya mizigo kutumia muda mwingi yanaondoka," alifafanua Kamwelwe.

Pia wanatafuta njia ya kutumia magari maalum yatakayokuwa yakisafirisha minofu ya samaki kwenda katika Bandari ya Dar es Saalam na Tanga.

"Minofu mingine tutakuwa tunatumia meli kuisafirisha, kwa kuwa wateja wapo wengi sana na bidhaa zetu zinahitajika sana katika soko la nje," alisema.



Ofisa Uchaguzi wa Jimbo la Dodoma Mjini, Albert Kasogi (katikati), akifungua mkutano wa ushawishi na utetezi kwa viongozi wa vyama vya siasa kuwajumuisha watu wenye ulemavu kwenye michakato ya uchaguzi mkuu wa 2020. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Mavunde asaidia vifaa ujenzi sekondari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAFUNZI wa shule za sekondari kwenye baadhi ya mitaa ya Kata ya Chahwa, Wilaya ya Dodoma, wanatembea umbali wa zaidi ya kilometa 10 kwa siku kufuata elimu eneo la Ipala na Mtumba, hali inayochangia kushindwa kufikia ndoto zao.

Kufuatia hali hiyo, Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, ameunga mkono jitihada za wakazi wa kata hiyo kwa kusaidia vifaa mbalimbali vya ujenzi wa shule ya sekondari ili kuondokana na adha hiyo.

Akisoma risala ya naibu huyo wakati wa uchimbaji wa msingi wa ujenzi wa shule hiyo itakayoitwa Mahoma Makulu, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mahoma Makulu, Emmanuel Yohana, alisema kutokana na kutembea umbali huo wanakutana na vishawishi vingi na baadhi kupata mimba.

Alisema wanafunzi wa sekondari wa mitaa ya Pembamoto, Chidefu na Homa Makulu, wanatembea umbali huo kwenda na kurudi jambo linalowaingiza kwenye vishawishi na kukatisha ndoto zao kielimu.

Alisema kutokana na adha hiyo waliamua kukubaliana kujenga shule na wenyeviti wa mitaa mitatu walitoa tofali 300 kila mmoja na mifuko 30 ya saruji.

"Tulipata kwa kumshirikisha mbunge ambaye alilikubali na sasa tumeanza ujenzi na wananchi wetu wamekuwa wakichanga kidogo kidogo pamoja na kutoa nguvu kazi kwa ajili ya ujenzi wa shule hii," alisema.

Kwa upande wake, Mavunde alisema ameamua kujenga shule hiyo kutokana na elimu kuwa mkombozi wa familia nyingi Dodoma na kusaidia kuachana na utaratibu wa kuwaozesha watoto.

Alisema ifikapo mwaka 2020/21 wanafunzi wataanza kusoma kwenye shule hiyo.

"Nawaunga mkono kwa kutoa mifuko ya saruji 100 na tofali 5,000 ili mwendelee na ujenzi na kikubwa tuendelee kujitolea kwa kuwa shule hii ni ya wananchi," alisema.

Mavunde alisema mchango huo ni sehemu ya ahadi yake aliyoitoa wakati akiomba kura 2015 na kuomba asitafsiriwe vibaya.

Naye, Ofisa Elimu Sekondari wa Jiji la Dodoma, Upendo Rweyumamu, alisema serikali itahakikisha shule hiyo inasajiliwa.

HABARI MBEYA



Wakazi wa Jiji la Mbeya wakikokota mikokoteni iliyosheheni majani ya kulisha mifugo, na kuwafanya washindwe kuona nyuma katika barabara kuu ya Tanzania na Zambia, eneo la stendi ya mabasi ya Nanenane, jijini humo juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani.. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# W'biashara waitwa TRA kukadiriwa kodi

**Mwandishi Wetu,** MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imewataka wafanyabiashara ambao hawajakadiriwa kodi ya mapato kwa kipindi kinachoishia Juni 30, mwaka huu kufika katika ofisi za mamlaka hiyo kukadiriwa na kulipa kodi zao kabla ya siku hiyo.

Kaimu Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Stephen Kauzeni, aliyasema hayo wakati wa kampeni ya uhamasishaji ulipaji kodi inayoendelea mkoani Mbeya.

Pia amewakumbusha wafanyabiashara wote ambao mwaka wao wa mahesabu unaishia Desemba 31, 2019 kuwasilisha ritani zao TRA kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Kauzeni alisema kwa wafanyabiashara wanaolipa kwa awamu, lakini hawajakadiriwa kodi zao ni vyema wakaenda TRA ili wakadiriwe na walipe mapema kabla ya tarehe ya mwisho kuepuka adhabu na riba.

"Tunawatembelea wafanyabiashara kwenye maeneo yao ya biashara ili kuwakumbusha na kuwahimiza wale ambao bado hawafanyiwa makadirio, wakakadiriwe na wawahi kulipa kodi zao kwa wakati bila bughudha kuliko kusubiri siku ya mwisho kabisa," alisisitiza.

Aliongeza kuwa kutokana na janga la ugonjwa wa Covid- 19, TRA isingependa kuona watu wengi wanakwenda katika ofisi zake kwa wakati mmoja kwa kuwa inaweza kusababisha msongamano, hivyo imebidi maofisa wa TRA waingie mitaani kuwafuata walipakodi kwenye biashara zao na kuwasisitiza wakalipe kodi kwa wakati kuepuka misongamano katika ofisi zake.

"Ni wajibu wa mlipakodi kulipa kodi zake kwa wakati, lakini TRA ina wajibu wa kutoa elimu ya kodi na vilevile kumkumbusha mlipakodi kulipa kodi zake kwa wakati, ndiyo maana tumekuja huku madukani kwao kuwapatia elimu ya kodi na kuwahimiza kulipa kodi kwa wakati," alisema.

Kuhusu wafanyabiashara ambao mwaka wa mahesabu unaishia Desemba 31, 2019, Kauzeni amewasisitiza kuhakikisha wanawasilisha ritani zao kabla au Juni 30, 2020 ili ritani zao ziweze kuhakikiwa na kufanyiwa kazi kwa wakati kama sheria za kodi zinavyotaka.

"Niwasihi walipakodi wafuate sheria ya usimamizi wa kodi na kuwasilisha ritani zao ziweze kufanyiwa kazi mapema."

Kampeni ya uhamasishaji ulipaji kodi kabla ya Juni 30, 2020 inalenga kuwakumbusha walipakodi kulipa kodi zao kwa wakati na kwa wiki hii inaendelea katika mkoa wa Mbeya na wilaya zake.

Kampeni hii pia imelenga kuongeza hamasa ya ulipaji kodi kwa hiari miongoni mwa wafanyabiashara na watoa huduma zinazolipiwa kodi kama mawakili, wahasibu na fani zingine zilizosajiliwa.

## Washereheshaji waaswa bei elekezi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa washereheshaji Mkoa wa Mbeya, Charles Mwakipesile, amewahimiza kuzingatia bei elekezi waliyokubaliana ili kuendelea kutunza heshima ya kazi yao.

Mwakipesile alitoa kauli hiyo juzi, kuwa siku kadhaa zimepita tangu Rais John Magufuli avunje Bunge mjini Dodoma, na kuagiza shule zote nchini zifunguliwe pamoja na shughuli zote ziendelee zikiwamo harusi na sherehe nyingine.

Kutokana na kauli hiyo, aliwatahadhari wenzake kuzingatia makubaliano yako kwamba mshereheshaji yeyote anatakiwa kufuata bei elekezi ambayo kima cha chini shilingi milioni moja kwa ukumbi wa kawaida na mkubwa ni Sh. milioni 1.5 na sio kukubali kulipwa kiasi kidogo ambacho kinashusha hadhi ya kazi hiyo.

"Tunampongeza Rais wetu kwa kuruhusu sherehe ziendelee kama kawaida, nawakumbusha ma-MC wenzangu tujitunzie heshima tuheshimu makubaliano yetu tuache njaa hata kama shughuli zilisitishwa, tulikubaliana yeyote atakayekiuka atakuwa amejiondoa kwenye umoja wetu," alisema Mwakipesile.

Pia aliwaomba wamiliki wa kumbi za hoteli kuwa na orodha ya washereheshaji wote ikiwa ni njia moja wapo ya kujitangaza kibiashara.

Aliongeza wateja wao wanapaswa kufahamu kuwa bei ya kuanzia shilingi milioni moja ni ndogo kwani wanalipa ushuru na nyingine inakatwa kwenye Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA).

Aidha, alipiga marufuku uvaaji holela wa mavazi ambayo yanashusha hadhi ya mshereheshaji kwa maelezo kuwa baadhi wamekuwa wakitia aibu kutokana na uvaaji wao ambao hauendi na wakati.

# WCS yabaini mazito hifadhi ya Kitulo, Mlima Rungwe

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

JUMLA ya vizalia 102 vya viumbe hai wakiwamo wanyama vimegunduliwa na shirika linalojihusisha na uhifadhi wa Mazingira la WCS katika maeneo ya Hifadhi ya Mlima Rungwe na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Miongoni mwa viumbe hao ni nyoka anayeangulia mayai tumboni kisha kutoa vifaranga.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa Elimu ya Mazingira wa WCS, Anthony Minazi, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na jitihada zinazofanywa na shirika hilo katika kuhifadhi viumbe hai mbalimbali.

Alisema katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo na Hifadhi ya Mlima Rungwe, kuna aina 102 za viumbe hai ambavyo vimeweza kugunduliwa tangu shirika hilo lianze kufanya kazi katika maeneo hao.

Mratibu huyo alisema katika utafiti uliofanywa na shirika hilo katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Rukwa wamebaini kuwapo kwa nyoka ambaye anaangulia mayai tumboni kisha kutoa vifaranga, ingawa shirika hilo linaendelea kumfanyia utafiti zaidi nyoka huyo kama anapatikana maeneo mengine duniani.

Alisema mbali na maajabu hayo, shirika hilo limebaini kuwapo kwa mbega wekundu katika msitu wa Mbizi uliopo mkoani Rukwa na kuwa aina kama hiyo inapatikana katika Msitu wa Jozani uliopo Zanzibar.

"Mbega hawa wekundu wanapatikana katika eneo la Mbizi mkoani Rukwa na katika Hifadhi ya Msitu wa Jozani Zanzibar na kuwa wanapatikana katika maeneo hayo tu duniani," alisema.

Pia alibainisha kuwa kuna nyani aina ya Kipunji (highland mangabey) ambaye anapatikana katika hifadhi pekee ya Mlima Rungwe na katika Hifadhi ya Taifa Udizungwa tu duniani na kuwa ni nyani wa kipekee kutokana na mwonekano mzuri.

Minazi alisema kutokana na uwapo wa viumbe hao, shirika hilo kwa kushirikiana na halmashauri husika wanajitahidi kutoa elimu juu ya uhifadhi wa mazingira na kuwa kuna jumla ya vijiji 40 ambavyo vipo karibu na maeneo ya hifadhi za misitu.

"Kuna vijiji zaidi ya 40 ambavyo tunashirikiana navyo katika kuhifadhi mazingira ikiwamo misitu na viumbe hai na kuwa katika Hifadhi ya Mlima Rungwe pekee kuna jumla ya vijiji 16, ambapo mpaka sasa kuna matokeo mazuri ya kuhakikisha viumbe hivyo vinahifadhiwa," alisema.

Alisema kuna baadhi ya viumbe vimetoweka katika maeneo yao ya asili kutokana na shughuli za kibinadamu na kuwa katika pori tengefu la Mbuzi lililopo Wilaya ya Nkasi kulikuwa na mbega wekundu ambao wameshatoweka na kuelekea kusikojulikana.

Alisema kuna jitihada za kuhifadhi mazingira kwa kupanda miche ya miti ikiwapo ya asili kwa ajili ya kuhakikisha viumbe hai vilivyopo katika maeneo hayo vinahifadhiwa kwa ajili ya kizazi kijacho.

# Bandari Mpigaduri yapigiwa chepuo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Mohamed Said Dimwa, ameitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Bandari ya Mpigaduri iliyopo Maruhubi, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Akisoma maoni ya kamati hiyo kwa bajeti ya serikali ya mwaka 2020-2021 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020-2021 haijaonyesha kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambao ni moja ya tegemeo la serikali kuingiza mapato.

Alisema Bandari ya Malindi imezidiwa na wingi wa shughuli zenye mchanganyiko ikiwamo usafiri wa huduma za abiria pamoja na mizigo ya makontena.

"Mheshimiwa Spika mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kutekeleza mradi wa Bandari ya Mpigaduri kwa kutumia fedha za ndani, lakini hadi sasa hakuna fedha zilizotengwa," alisema.

Aliitaka serikali kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la maabara ya utafiti wa maradhi ikiwamo ya kuambukiza ili kusaidia kupatikana kwa taarifa zake haraka.

Alisema tatizo la ukosefu wa maabara ya aina hiyo lilijitokeza hivi karibuni na serikali kulazimika kupeleka taarifa za uchunguzi wa vipimo vya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19, Tanzania Bara.

"Mheshimiwa tunahitaji haraka jengo la maabara ya kisasa ya uchunguzi wa maradhi mbalimbali ili tuweze kupata matokeo ya taarifa ya vipimo humu humu nchini na sio kusafirisha hadi Tanzania Bara," alisema.



Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu, Simai Muhammed Said, akiosha mikono yake kwa kutumia kitakasa 'sanitizer', wakati akiingia katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watangaza nia urais Z'bar watakiwa kujipima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema wagombea wa CCM wanaochukua fomu kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu ujao ni vyema wakawa na sifa zinazolingana na Rais Dk. Ali Mohamed Shein ikiwamo kuwa na busara, ustahimilivu, uaminifu na mapenzi kwa wananchi wake kwa ajili ya kuleta maendeleo na utulivu wa nchi.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2020-21, alisema kipindi cha miaka 10 ya Dk. Shein aliongoza nchi kwa kuweka maslahi mbele kwa wananchi wake.

"Dk. Shein anawajali wananchi wake ikiwamo wanyonge kwa kutekeleza fikra na dhamira ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964, ambapo elimu na sekta ya afya imetangazwa bure kwa wananchi wote," alisema Haroun.

Alisema katika kipindi chake michango yote ya shule waliyokuwa wakichangishwa wazazi imefutwa kwa lengo la kuwapunguzia mzigo wananchi na kuona wanafunzi wanapiga hatua kubwa ya maendeleo ya ufaulu wa masomo yao.

Alisema katika juhudi hizo serikali imeweka mazingira mazuri sekta ya elimu kwa kujenga shule za ghorofa zikiwa na vifaa kamili vya maabara pamoja na kupatikana kwa uhakika wa madawati kwa wanafunzi wake.

"Mimi niliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Madawati ambapo katika kipindi kifupi tumelipatia ufumbuzi tatizo hilo kwa kiwango kikubwa katika shule mbalimbali za Unguja na Pemba... nawapongeza Wawakilishi kwa kuchangia kila mmoja shilingi milioni tatu," alisema.

Alisema katika kipindi chake watumishi wa umma walipata mafanikio kwa kuongezwa mishahara mara nne pamoja na posho za watumishi na kupandishwa madaraja mbalimbali ikiwamo wafanyakazi waliokuwa na viwango vya chini vya elimu.

Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Issa Haji Ussi Gavu, alisema Dk. Shein atakumbukwa katika kipindi cha uongozi wake kulipatia ufumbuzi tatizo la nishati ya mafuta na gesi na Zanzibar kuwa na sheria yake kamili na rasilimali hiyo.

Alisema suala la mafuta na nishati ya gesi lilikuwa moja ya kikwazo kikubwa na kwa muda mrefu lilikuwa likizungumzwa, lakini halikupata ufumbuzi ikiwamo kuwapo kwa sheria ambayo sasa imetoa nafasi kwa Zanzibar kufanya utafiti wa utafutaji wa mafuta na gesi.

"Suala la mafuta na gesi lilikuwa moja ya changamoto kubwa na kuzungumzwa kwa muda mrefu, lakini Dk. Shein alikuja kulipatia ufumbuzi kwa kuwapo sheria kamili na leo hii tumefanya utafiti wa mafuta na gesi na tunasubiri matokeo yake," alisema.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Haji Omar Kheir, alimpongeza Dk. Shein kwa kufanikiwa kudumisha amani na utulivu wa nchi na kuwapo kwa mazingira mazuri ya uwekezaji.

"Katika kipindi cha miaka kumi tumeshuhudia amani na utulivu ukidumishwa kwa wananchi pamoja na wawekezaji kuwekeza katika miradi mbalimbali ikiwamo miradi ya ujenzi wa hoteli," alisema.

# Baraza lamwagiwa sifa kupitisha miswada 125

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Said Hassan Said, amesema katika kipindi cha miaka kumi ya uongozi wa Rais Dk. Ali Mohamed Shein, Baraza la Wawakilishi limevunja rekodi na kupitisha jumla ya miswada 125 yenye maslahi kwa wananchi wa Zanzibar.

Said, alisema hayo wakati akichangia bajeti ya serikali kwa mwaka 2020-2021 na kuwaaga wajumbe wa baraza hilo alikuwa mjumbe kwa kupitia nafasi yake ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Alisema Baraza limevunja rekodi ya kupitisha miswada hiyo ikiwamo wa mafuta na gesi ambao ulikuwa ukisubiriwa kwa hamu na wananchi wengi wa Zanzibar.

Mwanasheria Mkuu alisema kwa muda mrefu suala la mafuta na gesi pamoja na utafiti na uchimbaji wa rasilimali hiyo lilikuwa likizungumzwa na kutajwa, lakini halikupata ufumbuzi wa kisheria.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kipindi cha miaka kumi tumefanikiwa kupitisha jumla ya miswada 125 ya sheria ikiwamo wa mafuta na gesi ambao umeruhusu Zanzibar sasa kufanya utafiti wa rasilimali ya mafuta na gesi," alisema.

Aliwataka wananchi kuwa na subira na matokeo ya utafiti uliofanywa wa mafuta na gesi, hatima yake itajulikana na kujulishwa wananchi wote wa Zanzibar.

Alisema sheria nyingi zilizofanyiwa marekebisho zinatokana na kilio cha wananchi wanaowakilishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Serikali kusikiliza mapendekezo hayo na kuzifanyia marekebisho.

Kadhalika, sheria ya vileo imefanyiwa marekebisho ambayo kwa muda mrefu ilikuwa ikilalamikiwa kwa kuwapo kwa utitiri wa nyumba za starehe katika maeneo wanayoishi wananchi na kuharibu mila na silka za wananchi ikiwamo vijana.

Alikiri sheria ya vileo ilikuwa ya zamani tangu enzi za ukoloni ambayo imepitwa na wakati na hailingani na mazingira ya sasa yanayozingatia ubinadamu mila, silka na utamaduni.

"Sheria ya vileo imefanyiwa marekebisho baada ya malalamiko mengi kutoka kwa Wawakilishi yanayotoka kwa wananchi katika majimbo...serikali imesikia kilio hicho na kuifanyia marekebisho sheria hiyo," alisema.

# Viongozi wa dini wawafunda wananchi uchaguzi

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

VIONGOZI wa dini mkoani Dodoma wamewaomba Watanzania kuchagua viongozi wenye uthubutu wa kuchukua uamuzi mgumu na uadilifu ili taifa liweze kustawi kwa amani.

Hayo yalielezwa jana jijini hapa na viongozi hao wakati wakitoa tamko la kumpongeza Rais John Magufuli na serikali ya awamu ya tano.

Akitoa tamko hilo, Askofu wa Kanisa la EAGT Ipagala, Evance Chande, alisema nchi inapokwenda kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu, ni vyema Watanzania wakazingatia kuchagua viongozi wenye uthubutu huo.

Alisema Rais Magufuli ni kiongozi mwenye kusimamia haki inayozaa tunda la amani katika Taifa la Tanzania.

"Ni kweli mwenye haki akiongoza, watu hufurahia matunda yake kama sote tulivyosikia na kuona kwa macho yetu. Hivyo Mungu ambariki kiongozi wetu," alisema.

Alimpongeza Rais Magufuli kwa kufanikisha miradi mikubwa ya kimkakati kufanyika mkoani Dodoma.

Alisema pia wanampongeza, Rais Magufuli jinsi alivyopambana na madawa ya kulevya, kufufua uchumi pamoja na jinsi alivyopambana na ugonjwa wa corona.

"Sisi kama viongozi wa dini tumefarijika sana kwani kuna mabadiliko makubwa yametokea katika mkoa wa Dodoma," alisema.

# WLAC yatoa elimu polisi madawati ya jinsia

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC), kimeanza kutoa mafunzo kwa maofisa wa madawati ya jinsia ya Jeshi la Polisi ambayo yanayohusika na upokeaji wa kesi za ukatili wa kijinsia jijini Dar es Salaam.

Jeshi hilo pia limesema matukio yanayoripotiwa zaidi katika madawati hayo ni malalamiko ya malezi ya watoto, kubakwa na kulawitiwa.

Mrakibu Mwandamizi wa Polisi na Mkuu wa Dawati la Jinsia Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Leah Mbunda, alisema vitendo hivyo vilikuwa vikifanywa zaidi na wasaidizi wa nyumbani.

Alisema katika miezi mitatu ambayo wanafunzi walikuwa wamefunga shule kutokana na tishio la ugonjwa wa corona, idadi ya vitendo vya ukatili kwa watoto vilivyoripotiwa katika madawati hayo viliongezeka kwa kasi.

"Sababu ya kuongezeka kwa vitendo hivi katika kipindi cha corona ni watoto kushinda nyumbani kwa muda mwingi na kufanyiwa vitendo hivyo na wasaidizi wa nyumbani wakati wazazi wao wakiwa wamekwenda katika mihangaiko ya kutafuta riziki," alisema Mbunda.

Mbunda alisema matukio ya kulalamikia malezi ya watoto, kubwakwa na kulawitiwa, yamekuwa yakitokea zaidi katika maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu pamoja na maeneo ya makazi ya watu wenye kipato cha chini.

"Kwa sasa wananchi wamehamasika zaidi kuripoti matukio ya ukatili katika madawati ya jinsia tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma na malalamiko ya walezi ya watoto, kubakwa kwa watoto na kulawitiwa ndiyo yamekuwa yakiripotiwa kwa wingi."

"Mafunzo haya ni muhimu sana kwetu kwa sababu tunashughulika na mambo ya sheria, askari wanaofanya kazi katika madawati haya wakipata uelewa wa sheria, inakuwa rahisi katika utendaji wao wa kazi na utoaji haki kwa kufuata misingi hiyo ya sheria," alisema Mbunda.

Mkurugenzi Mtendaji wa WLAC, Theodosia Nshala, alisema wamelenga kutoa mafunzo kwa kundi hilo kwa sababu ya nafasi kubwa waliyonayo ya kufanikisha utoaji wa haki kwa kesi zinazohusiana na vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia.

Alisema bado kuna wimbi kubwa la vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia na kwamba kuendelea kutoa elimu kwa kundi hilo ni muhimu ili kufanikisha kazi ya kupambana navyo.

"Tumeamua kutoa mafunzo kwa maofisa wa polisi wanaofanya kazi katika madawati ya jinsia kwa lengo la kuwajengea uwezo wa sheria ili kuboresha huduma ya utoaji haki pamoja na kutatua matatizo mbalimbali ambayo yanaripotiwa katika madawati yao yaliyopo katika vituo vya polisi," alisema Nshala.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa tatu kushoto), akikagua mashamba ya maonyesho wakati wa hafla ya ufunguzi wa Maonyesho ya Kilimo Biashara mwaka 2020, yaliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI-Ilonga) kwa kushirikiana na kampuni ya mbegu wilayani Kilosa mkoani Morogoro, juzi. **PICHA: WIZARA YA KILIMO**

# Waandishi waaswa kufuata maadili

**Na Enock Charles**

WAANDISHI wa habari wameaswa kuzingatia maadili ya uandishi wa habari na kutokukubali kuingia katika mitego ya wanasiasa.

Pia, wametakiwa kufuata misingi ya uandishi wa habari katika kuhabarisha jamii kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza katika mkutano wa waandishi wa habari, uliofanyika kwa njia ya mtandao jana na kuratibiwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Jumuiya ya Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Ananilea Nkya, alisema ili kujenga heshima katika tasnia ya habari nchini ni muhimu waandishi kuepuka rushwa.

"Ukiwa mwandishi wa habari ukawa unafungamana na chama huwezi kufanya kazi yako vizuri, utafanya kazi kwa maslahi binafsi,"alisema Nkya.

"Historia itatuhukumu kama wanahabari ninatamani mwaka huu media (tasnia ya habari), tusimame kama fourth estate (mhimili wa nne wa dola)," aliongeza.

Alisema waandishi kufuata maadili ni wajibu wa msingi na kwamba kutawezesha vyombo vya habari kuwa na nguvu ya kuwasemea wananchi, bila kujali tofauti mbalimbali zilizopo katika jamii katika misingi ya vyama vya siasa, itikadi, imani za kidini au kabila.

Naye, Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa, akichangia mjadala huo alisema kuwa ni muhimu waandishi wa habari wakatafuta mtu sahihi wa kuzungumza pale linapotokea jambo ili kuepuka kuingia katika mitego ya wanasiasa na kuandika maoni ya mtu binafsi.

"Waandishi wanatakiwa kutofautisha maoni ya mtu binafsi na ukweli, tafuta ukweli wa jambo na kuhakikisha kinachoandikwa ni sahihi," alibainisha Ngurumwa.

# HABARI KIMATAIFA

## Madaktari hospitali za umma waendeleza mgomo

**LAGOS, Nigeria**

ASILIMIA 40 ya madaktari katika hospitali za umma nchini Nigeria wanaendelea na mgomo walioanza mwanzoni mwa wiki.

Hata hivyo, madaktari ambao hawajajiunga na mgomo huo ni wale wanaohudumia wagonjwa walioathirika na corona.

Mgomo huo unakuja wakati nchi hiyo inaendelea kurekodi visa vya maambukizi na vifo vinavyotokana na ugonjwa wa virusi vya corona.

Hadi jana, Nigeria imerekodi wagonjwa 17,148 vya maambukizi ya virusi vya Corona, baada ya visa vipya 573 kuthibitishwa.

Aidha, wagonjwa 5,623 wamepona na watu 455 wamefariki dunia kutokana na kuugua ugonjwa wa virusi vya corona.

Jana watu wanne walithibitishwa kufariki kwa mujibu wa vyanzo vya hospitali nchini Nigeria.

Madaktari nchini humo wanaomba uwezo zaidi katika kufanya kazi yao ipasavyo, huku wakibaini kwamba wanahatarisha maisha yao kwa kufanya kazi bila ulinzi zaidi katika kazi yao.

Madaktari hao wanaomba serikali kufanya jitihada za kuhakikisha maslahi yao wanayodai yanapatiwa ufumbuzi.

RFI

**Madaktari nchini humo wanaomba uwezo zaidi katika kufanya kazi yao ipasavyo, huku wakibaini kwamba wanahatarisha maisha yao kwa kufanya kazi bila ulinzi zaidi katika kazi yao.**

# Changamoto sita zinazomsubiri Rais mpya Burundi kuzitatua

**BUJUMBURA, Burundi**

RAIS mpya wa Burundi, Jenerali Evariste Ndayishimiye, alichukua rasmi mamlaka ya urais nchini Burundi jana, baada ya kutangazwa mshindi mwanzoni mwa mwezi huu.

Jenerali Ndayishimiye alipata ushindi kupitia chama tawala cha CNDD-FDD kwa asilimia 68.72% ya kura zilizopigwa.

Licha ya kushinda kiti hicho, atakabiliana na changamoto kubwa sita akiwa kama kiongozi wa Taifa hilo.

Jenerali Evariste Ndayishimiye, amechukua nchi yenye mgawanyiko mkubwa kutoka kwa kiongozi wa zamani, Pierre Nkurunziza, ambaye alifariki mwezi huu.

### UKABILA

Nchi ya Burundi inakabiliwa na migawanyiko tofauti, ikiwamo ya ukabila baina ya Watuhu na Watutsi, mgawanyiko wa kisiasa baina ya serikali na upinzani.

### MZOZO WA WAKIMBIZI

Jenerali Ndayishimiye pia anarithi nchi yenye mzozo mkubwa wa wakimbizi uliosababishwa na vita na ghasia za mauji za muda mrefu nchini Burundi.

Ghasia za kisiasa na kiusalama pamoja na mzozo wa kiuchumi uliosababishwa na Burundi kuwekewa vikwazo na Umoja wa Mataifa (UN) zimewalazimisha zaidi ya wananchi 350,000 kukimbilia nchi jirani na wengine 110,000 ni wakimbizi wa ndani ya nchi.

Hata hivyo hakuingilia kati kuzuwia ghasia zilizoikumba Burundi kufuatia uchaguzi wenye utata uliomuweka madarakani mwaka 2015.

Wakimbizi wa Burundi watasubiri kuona iwapo Jenerali Ndayishimiye atatoa mazingira salama yatakayowawezesha kurejea na kuishi tena nchini mwao.

### KUWARIDHISHA MAJENERALI

Moja ya changamoto kubwa ya urais anayotarajiwa kukabiliana nayo kushughulikia maslahi ya watu binafsi ndani ya chama tawala cha CNDD-FDD.

Ushindi wa Ndayishimiye umetokana na historia yake ya kijeshi katika CNDD-FDD.

Alishinda kwasababu alikua ni mgombea wa chama tawala kwa kupata uungaji mkono wa baadhi ya majenerali wenye nguvu ndani ya chama.

Ikizingatiwa kuwa hakuwa chaguo la mtangulizi wake, Pierre Nkurunziza, kama rais ambaye chaguo lake lilikuwa ni Pascal Nyabenda- Spika wa bunge, itamlazimu Jenerali Ndayishimiye kuwarai wafuasi wa mtangulizi wake ambao walikua na chaguo la mtu mwingine kwa misingi ya kuepusha mpasuko ndani ya CNDD-FDD.

### MZOZO WA KIUCHUMI

Tangu mwaka 2015, Burundi imeshuhudia kuzorota kwa uchumi. Viwango vya umaskini vimepanda hadi kufikia asilimia 74. Burundi kwa sasa ni nchi ya tatu maskini zaidi duniani.

Ndayishimiye atatakiwa kushughulikia viwango vya juu vya ukosefu wa ajira na umaskini mkubwa. Wahisani wengi wa kimataifa wamesitisha msaada wao kwa Burundi baada ya uchaguzi wa 2015, jambo lililosababisha uhaba mkubwa wa fedha za kigeni.

### UHUSIANO KIMATAIFA

Jenerali Ndayishimiye atatakiwa kurejesha uhusiana na mataifa ya Ulaya, pamoja na Marekani ambayo yaliiwekea Burundi vikwazo kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu, uliofuatia ghasia zilizoibuka wakati na baada ya uchaguzi wa urais wa mwaka 2015.

### UHUSIANO NA MAJIRANI

Jenerali Ndayishimiye atatakiwa kurejesha uhusiano mwema na taifa jirani la Rwanda, ulioharibika enzi ya mtangulizi wake Pierre Nkurunziza.

Nchi mbili zimekua zikishutumiana kila moja kuhatarisha usalama kwa kuwahifadhi wapinzani wa nchi zao.

Licha ya kutegemeana kiuchumi na kuwa na historia zinazofanana, uhusiano wa nchi hizi mbili ni wa kihistoria kwani zilikua himaya moja kabla ya kutenganishwa na mkoloni.

Baada ya kifo cha Rais Nkurunziza, Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alituma rambirambi kwa Warundi uliokua ni ujumbe wake wa kwanza wa umma kwa nchi hiyo jirani, tangu uhusiano wa Rwanda na Burundi ulipoingia dosari mwaka 2015.

***BBC***



Waandamanaji nchini Marekani wakiwa mbele ya White House mjini Washington, DC kulaani vitendo vya kikatili na ubaguzi vinavyofanywa na baadhi ya polisi. **PICHA: AFP**

# Kenya, Djibouti zachuana kupata nafasi UN

**NEW YORK, Marekani**

MCHAKATO wa kupata kiti katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa umeendelea huku nchi za Kenya na Djibouti zikishindwa kupata kura za kutosha.

Kwenye mchakato huo Kenya ilipata kura133 dhidi ya Djibouti iliyozoa kura 78, na hivyo nchi zote mbili kushindwa kupata theluthi mbili ya kura zote, kama inavyohitajika, ili kushinda kiti kisicho cha kudumu kwenye baraza hilo.

Nchi hizo mbili zinatarajiwa kuingia kwa duru ya pili ya uchaguzi huo, ili kumtafuta mshindi, atakayeshikilia nafasi hiyo kwa miaka miwili.

Nchi zingine za Mexico, India, Ireland na Norway zilichaguliwa lakini itapaswa mataifa yote 193 ya Umoja huo, kukutana tena ili kujaza pengo lililobaki baada ya Kenya, ambayo ilikuwa imepata uungwaji mkono wa Umoja wa Afrika (AU), kutopata idadi ya kura zilizohitajika.

Djibouti ilikataa kuheshimu uamuzi wa AU na kuamua kuendelea na mchakato wa kampeni ya kutafuta uungwaji mkono kutoka kwa nchi mbalimbali.

Kwa sasa, Afrika inawakilishwa na nchi za Niger, Tunisia na Afrika Kusini kwenye baraza hilo. Hata hivyo, awamu ya Afrika Kusini inafika kikomo mwishoni mwa mwaka huu na nafasi yake ndiyo inayopiganiwa na Djibouti na Kenya.

Wakati huohuo, Canada ilishindwa na Ireland na Norway kwenye uchaguzi uliokuwa na ushindani mkali uliosababisha Ireland kuomba usaidizi wa mwanamziki maarufu, Bono.

Mexico na India zilichaguliwa bila kupingwa. Mataifa mapya kwenye baraza hilo lenye wajumbe 15 yataanza muhula wao wa miaka miwili Januari mosi, mwakani.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ni chombo muhimu zaidi kwenye mfumo wa Umoja huo, kwani lina nguvu za kufanya uamuzi wenye uzito mkubwa kimataifa.

Baraza hilo lina wanachama wa kudumu watano: Marekani, China, Russia, Ufaransa na Uingereza, ambao kila mmoja ana kura ya turufu. ***VOA***

## HABARI MICHEZO




# LUIZ
## AKUBALI LAWAMA KIPIGO CHA ARSENAL

**LONDON, England**

DAVID Luiz amekubali kubeba lawama zote kwa kichapo cha Arsenal ilichokipata kutoka kwa Manchester City, akidokeza kwamba alitakiwa kumaliza sakata la majaliwa yake kabla ya msimu kuendelea tena.

Mlinzi huyo wa kimataifa wa Brazil alikuwa na wakati mgumu katika kipindi cha kwanza pale kwenye dimba la Etihad Jumamosi wakati Arsenal ikikubali kichapo cha mabao 3-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England.

Bao la kwanza lililofungwa na Raheem Sterling lilitokana na makosa ya Luiz kabla ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumdondosha Riyad Mahrez mwanzoni mwa kipindi cha pili, na Kevin De Bruyne akafunga kwa penati, kabla ya Phil Foden kuifungia City la tatu dakika za majeruhi.

Luiz mwenye umri wa miaka 33, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, amekubali kulaumiwa kwa kipigo hicho cha Arsenal kwenye mchezo wao huo wa kwanza tangu kurudi kwa ligi baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

"Ni makosa yangu, yalikuwa ni makosa yangu," alisema Luiz akiiambia Sky Sports.

"Nlitakiwa kuchukua uamuzi mwingine miezi miwili iliyopita, lakini sikufanya hivyo. Nafikiri timu ilifanya vizuri, hasa wakati walipokuwa watu 10 uwanjani, kocha ni mtu wa aina yake pamoja na wachezaji wote walicheza kwa kujituma, ni kosa langu."

Huku majaliwa yake yakiwa bado hayajulikani, Luiz amebainisha kama angefanya uamuzi mapema kuhusu mkataba wake pengine ingesaidia kuimarisha kiwango chake.

"Ni umuzi tofauti, kujaribu kuamua kuhusu majaliwa yangu ya baadae, nilijaribu kuamua mapema inavyowezekana, lakini ilishindikana," amesema.



## GATTUSO: "MUNGU WA SOKA" AMEIPA UBINGWA NAPOLI

**MILAN, Italia**

GENNARO Gattuso anahisi kujituma kwa bidii kwa Napoli ndio kumewafanya wazawadiwe na "Mungu wa soka" wakati wakiwafunga Juventus kwenye fainali na kushinda kombe la Coppa Italia.

Napoli ilitwaa taji hilo Jumatano kwa mikwaju ya penalti baada ya mchezo kumalizika kwa sare ya bila kufungana, huku Paulo Dybala na Danilo wakikosa penalti zao wakati Napoli ikiibuka kwa ushindi wa 4-2.

Hilo lilikuwa taji la kwanza kwa Gattuso kama kocha, na aliiambia Rai Sport: "Yeyote anayefanya kazi, lazima aiheshimu.

"Tunababahati. Ndio maana ninapata hasira; kunatakiwa kuwa na ari, heshima na umakini.

"Kuna Mungu wa soka ambaye anatoa zawadi kwa wale wote wanaofanya kazi kwa bidii."

Dakika chake baada ya Napoli kupata mafanikio hayo, Gattuso alikumbuka kifo cha dada yake Francesca, ambaye alifakiri dunia kwa sarakati mwanzoni mwa mwezi huu.

"Soka la Dunia limenipa zaidi ya kile nilichostahili," alisema. "Lakini mara zote unatakiwa kufikiria kuhusu familia kwanza. Katika maisha kile kilichotokea kinakuwa na maana kubwa zaidi."

Gattuso sasa anatarajia kuiongoza Napoli kwenye mechi zilizobaki za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ambapo wanashika nafasi ya sita kwenye msimamo wakipitwa pointi tisa na wanaoshika nafasi ya nne, Atalanta.

"Tuna kazi ya kucheza kwenye mechi 12 zilizobaki na tunaliheshimu hilo," alisema Gattuso.

# Zidane: Real Madrid inafuraha na Hakimi

**MADRID, Hispania**

REA Madrid inafurahishwa na kiwango cha Achraf Hakimi anachokionesha kule Borussia Dortmund, kocha mkuu Zinedine Zidane amesema.

Achraf mwenye umri wa miaka 21, alijiunga na Dortmund kwa mkataba wa mkopo wa miaka miwili mwaka 2018 na sasa mlinzi huyo amekuwa akijadiliwa sana kutokana na kiwango chake katika klabu hiyo ya Bundesliga.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco anatarajia kurudi Madrid, lakini amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Bayern Munich.


Zidane amesema amefurahishwa na kile alichokuwa anakifanya Achraf, ambaye amecheza mechi 17 kwa Madrid kabla ya kuondoka, na ameonesha kiwango cha kuvutia zaidi Dortmund.

Tunajua nini anachokifanya msimu huu, na nina furaha sana na kiwango chake, kwa sababu mwisho wa siku alihitaji kwenda nje kucheza, kucheza mechi nyingi na hicho ndicho anachokifanya," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafikiri sisi wote hapa (Madrid), na pale (Dortmund), tuna furaha na yeye Hakimi."



## HABARI MICHEZO



# FELIX APAGAWA KWA FURAHA KUFUNGA MAWILI

**MADRID, Hispania**

JOAO Felix amefurahishwa na kiwango chake wakati akifunga mabao mawili kuiwezesha Atletico Madrid kuibuka na ushindi wa 5-0 dhidi ya Osasuna kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Jumatano.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 20 alifunga mara mbili kabla ya mabao kutoka kwa Marcos Llorente, Alvaro Morata na Yannick Carrasco kuipa Atletico ushindi huo wa kuvutia.

Felix sasa amefikisha mabao nane kwenye msimu wake wa kwanza pale Atletico na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amebainisha kufurahishwa sana na kiwango chake.

"Najisikia vizuri na nina furaha sana kwa sababu ya mabao yangu mawili na ushindi wa 5-0," alisema Felix akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

Aliongeza: "Ni tofauti sana. Tunapenda kucheza na mashabiki wakiwa majukwaani, hata kama ni ugenini. Tunatakiwa kuzoea na kuendelea na hali hii."

Atletico ilijivuta hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi, ikiipia pointi mbili Real Sociedad - ambao wana mchezo mmoja mkononi - na Getafe.

"Kwa uhakika kabisa nina furaha sana, na nina amini kiwango changu hiki kitaendelea kuwa kwenye ubora wangu."

Atletico watarudi tena uwanjani wakicheza nyumbani dhidi ya Real Valladolid, Jumamosi.

# RONALDO, MASTAA WA JUVE WAMKASIRISHA SARRI

**TURIN, Italia**

MAURIZIO Sarri anaamini Cristiano Ronaldo na nyota wengine wa Juventus wanakosa "makali" baada ya kufungwa kwenye fainali ya kombe la Coppa Italia, Jumatano.

Napoli waliibuka na ushindi wa jumla ya penalti 4-2 dhidi ya Juve baada ya kutoka sare ya bila kufunga kwenye mchezo huo uliopigwa jijini Roma nchini Italia.

Katika mechi mbili tangu irudi kwenye michezo baada ya mlipuko wa virusi vya corona, Juve imekuwa haina uwezo wa kufunga mabao.

Sarri amesema Ronaldo na washambuliaji wengine wanatakiwa kuwa fiti zaidi baada ya kutokuwa dimbani kwa zaidi ya miezi mitatu.

"Hana makali kama ilivyo kwa Paulo Dybala na Douglas Costa, bado hayuko fiti kufanya kazi anayotakiwa kwa ubora wake," alisema akiiambia televisheni ya RAI.

"Sikusema zaidi kwa wachezaji baada ya mchezo. Nilikuwa na hasira na niliyevurugwa kama wao, hivyo kwa wakati huu ni bora kukaa kimya. Tutazungumza zaidi kesho asubuhi."

Paulo Dybala na Danilo walikosa penalti kwa Juventus, ambao wanaongoza msimamo wa Serie A kwa pointi moja kuelekea kwenye mchezo wake dhidi ya Bologna, Jumatatu.

# Fainali ya Uefa inaweza kuruhusu mashabiki



**LISBON, Ureno**

RAIS wa Shirikisho la Soka la Ulaya, UEFA, Aleksander Ceferin hajaondoa uwezekano wa mashabiki kuhudhuria fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa msimu huu.

Chombo hicho kinachosimamia soka la Ulaya kilithibitisha Jumatano kwamba, robo fainali na nusu fainali ya mashindano yote mawili zitafanyika Agosti.

Ligi ya Mabingwa itamalizikia jijini Lisbon nchini Ureno kati ya Agosti 12 hadi 23, huku katika miji ya Cologne, Duisburg, Dusseldorf na Gelsenkirchen nchini Ujerumani ndiko michuano ya Ligi ya Europa itakakochezewa kuanzia Agosti 10 hadi 21.

Mpango wa sasa ni kucheza mechi moja ya mashindano hayo, huku milango ikiwa imefungwa bila kuruhusu mashabiki, ingawa Ceferin amewaambia waandishi wa habari kwamba kama maambukizi ya virusi vya corona yataendelea kupungua wataangalia uwezekano wa kuruhusu mashabiki uwanjani.

"Kama ningejibu leo, pengine tunaweza kuwa na mashabiki uwanjani kwa Ligi ya Europa na Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali, nusu fainali na fainali," amesema.

Mwisho.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BARCELONA YAJIANDAA KUMPA LIONEL MESSI MKATABA MPYA

●●●Neymar pia atajwa kurudi Camp Nou, lakini bei inaweza...

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA inaonekana inaweza kumwongeza mkataba mpya nyota wake, Lionel Messi, amesema makamu wa raia wa zamani wa klabu hiyo, Emili Rousaud.

Pi amesema kwamba, miamba hao wa Ligi ya Hispania wanaweza kumsajili tena Neymar kipindi hiki cha majira ya joto.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina mkataba wake pale Camp Nou unamalizika mwaka 2021.

Imeripoti kwamba, Messi bado hajakubali kuongeza mkataba mpya baada ya kutokea kutoelewana na baadhi ya watendaji wa Barca.

Tayari ofa zimeanza kutoka nchini Italia kwa Klabu ya Inter Milan na wababe wa Ligi Kuu ya England, Manchester City, linapokuja suala la kutaka kumsajili nyota huyo.

Hata hivyo, Messi mwenyewe alidai kwamba, madai ya kuhusishwa na Inter yalikuwa ya uzushi.

Inaeleweka kwamba, miamba hao wa Katalunya wanajiamini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 ataongeza mkataba wake pale Barcelona kutokana na wa sasa kuelekea mwisho.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, Mtendaji huyo wa zamani wa Barca amedai kwamba litakuwa jambo la kushangaza kama Messi hataongeza mkataba pale Camp Nou.

Rousaud pia anamini kwamba Barcelona wanaweza kumsajili mchezaji wake wa zamani, Neymar kwa kiasi kidogo cha fedha kutokana na matatizo ya kifedha yaliyolikumba soka sababu ya mlipuko wa virusi vya corona.

Katika mahojiano, Rousaud amesema, "nafikiri Messi na Barcelona watafikia makubaliano ya kuongeza mkataba mpya, pande hizo mbili zinatakiwa kufanya makubaliano, lakini nitashangaa sana kama habari hiyo nzuri haitaendelea zaidi.

"Nafikiri inawezekana Neymar anaweza kurudi kipindi cha majira ya joto. Kwangu mimi naona kabisa jambo hili linawezekana kwa kiasi kikubwa.

"Nina hisia kwamba, mlipuko huu wa corona utasababisha bei ya mchezaji kushuka kwa kasi."

Messi alionekana kutofautiana na baadhi ya wajumbe wa bodi ya Barca kutokana na matokeo ya timu hiyo.

## KWA UFUPI

**CHELSEA YATAKA KUMSAJILI HAVERTZ**

CHELSEA inataka kumsajili kiungo mshambuliaji wa Ujerumani na Bayer Leverkusen, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21 na wapo tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 70, ingawa klabu hiyo ya Bundesliga imemthaminisha kwa pauni milioni 90. ***(Telegraph)***

**PEDRO AKUBALI KWENDA ROMA**

FOWADI wa Hispania, Pedro mwenye umri wa miaka 32, amekubali kujiunga na AS Roma kwa uhamisho huru na lazima aamue kama atasaini mkataba wa muda mfupi kukaa pale Chelsea hadi mwishoni mwa msimu huu. ***(Guardian)***

**JIMENEZ AFURAHIA KUHUSISHWA MAN U**

STRAIKA wa Wolves na Mexico, Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 29, amesema uvumi wa kumhusisha na Manchester United na Liverpool umemhamasisha kuimarika zaidi huku malengo yake ni kuhamia kwenye klabu kubwa. ***(Bolavip via Mirror)***

**FRASER AWAGOMEA BOURNEMOUTH**

KIUNGO wa Scotland, Ryan Fraser mwenye umri wa miaka 26 anataka zaidi ya pauni 100,000 kama ada kwa kuwa ni mchezaji huru, baada ya kukataa kuongeza mkataba wa muda mfupi kuendelea kukaa pale Bournemouth kwa kipindi cha msimu kilichobaki. ***(The Times)***

**KEITA TAYARI KWENDA AC MILAN**

KIUNGO wa Liverpool na timu ya taifa ya Guinea, Naby Keita mwenye umri wa miaka 25, yupo tayari kuungana na kocha wake wa zamani wa RB Leipzig, Ralf Rangnick katika klabu ya AC Milan kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A. ***(Milan Live via Express)***

**LEICESTER WAKATAA KUMUUZA CHILWELL**

KLABU ya Leicester City hawataki kumuuza mlinzi wake wa kushoto Muingereza, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 23 katika dirisha lijalo la usajili - hata kama watapewa ofa ya pauni milioni 50. ***(Sky Sports)***

**BAYERN KUMUUZA ALABA**

BAYERN Munich itafikiria kumuuza mlinzi wake wa kushoto, David Alaba mwenye umri wa miaka 27 raia wa Austria, kuliko kumuacha amalizie mkataba wake ili aondoke akiwa huru. ***(Telegraph)***

**ATERTA AOMBA KUSAJILI ARSENAL**

KOCHA Mikel Arteta ameiomba bodi ya Arsenal kumuunga mkono kwenye dirisha la usajili baada ya wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Chelsea kukubali kumsajili straika wa Ujerumani, Timo Werner kutoka RB Leipzig kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 54. ***(Mirror)***

**BENJAMINI KUTUA RB LEIPZIG**

BEKI wa kulia Monaco, Benjamin Henrichs, mwenye umri wa miaka 23 raia wa Ujerumani - ambaye anawaniwa na Bayern Munich - pengine atajiunga na RB Leipzig. ***(Bild Sport)***

**ROBINSON AGOMBEWA WEST HAM, BROM**

KLABU za West Ham na West Brom zinamfuatilia kwa karibu, mlinzi wa kushoto wa Wigan na Marekani, Antonee Robinson mwenye umri wa miaka 22. ***(Express and Star)***

**NANI AMUOTA RONALDO MAREKANI**

NAHODHA wa Orlando City ya nchini Marekani, Nani mwenye umri wa miaka 33, amesema mshambuliaji wa Juventus na nyota wa zamani wa Manchester United na mchezaji mwenzake wa timu ya taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye miaka 35, pengine atakwenda kucheza kwenye Ligi Kuu ya Marekani kabla ya kustaafu soka. ***(ESPN)***

HABARI MICHEZO

# KLABU ZATOA MASHARTI KUENDELEA NA LIGI KUU

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KLABU tisa za Ligi Kuu ya Zanzibar zimeliandikia barua shirikisho la soka Zanzibar, ZFF, kuelezea mahitaji wanayohitaji ili kuendelea na ligi ambayo ilisimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Klabu hizo ni Chuoni FC, Mlandege, Malindi, Jang'ombe boys, Chipukizi, Machomanne, Jamhuri, Mwenge na Selem View.

Klabu hizo zimeelezea kwamba, zinakabiliwa na changamoto kama viatu vya wachezaji, mishahara na posho kwa wachezaji pamoja na walimu, usafiri wa kila siku ya mazoezi, usafiri Unguja na Pemba, kambi siku za mechi na makazi ya wachezaji kwa timu zilizotoa wachezaji kutoka Tanzania bara na kisiwani Pemba.

Barua hiyo imesema, klabu zinakumbwa na hali ngumu ya kifedha hasa katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona.

"Kupitia mikutano miwili tuliyoifanya ukiwamo mmoja wa Mei 21 ulioitishwa na umoja wa Klabu pamoja na mkutano wa June 3, uliowashirikisha wajumbe wote wa kamati tendaji,tulitoa maadhimio yao kusaidiwa ili kurudi katika ligi hiyo," ilisema sehemu ya barua hiyo.

Aidha barua hiyo imeomba kufanyika kwa mkutano mkuu wa dharula ili kujadili changamoto hizo kabla ya kuendelea na ligi kuu iliyopangwa kuanza kutimua vumbi June 24 katika kituo cha Unguja pekee.

Akizungunza na Nipashe kaimu katibu wa ZFF, Ali Ame Vuai amekiri kupokea barua hiyo na kuwaomba kila timu iandike barua kivyake badala ya kuleta barua ya pamoja kama walivyofanya hivi sasa.

Aidha alisema kuwa Wizara ya michezo kushirikiana na ZFF inaendelea kuchukua jitihada kuona namna gani klabu hizo zitasaidiwa katika kipindi hiki ambacho kinajulikana kuwa ni kigumu ili kuona timu hizo zinamaliza msimu.

Mapema mwezi huu, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein alitoa kiasi cha Sh. milioni 21 kusaidia klabu ili kuendelea na ligi hiyo katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid -19.



Mchezaji wa timu ya Kitunda FC, Shabani Issa (kulia), akimtoka mchezaji mwenzake, Abas Nurdin, wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba, Yanga zagombania straika KMC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU za Simba na Yanga zimeingia kwenye vita kali ya kumgombea straika hatari wa KMC, Charles Ilamfya ambaye kwa siku za hivi karibuni amekuwa mwiba mchungu kwa timu hizo.

Meneja wa mchezaji huyo, Sharrif Majisafi amesema klabu hizo zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili, ingawa bado ana mkataba wa klabu yake ya KMC.

"Baadhi ya watu kwenye hizi klabu kubwa za Simba na Yanga wamekuwa wakinipigia simu kuniulizia kama wanaweza kumpata mchezaji wangu. Mimi nasema huyu kwanza bado ana mkataba na KMC, lakini hiyo haijalishi kama timu itaamua kuununua mkataba wake uliobaki," alisema.

Majisafi alisema katika timu hizo mbili, Yanga ndiyo inaonekana inamuhitaji zaidi mchezaji huyo kuliko wenzao wa Simba kwa sababu wao mara kwa mara ndiyo wamekuwa wakimuulizia.

"Na siyo timu hizo tu, mchezaji wangu ana ofa zingine nje ya nchi, kuna klabu ya daraja la pili nchini Ufaransa inamhitaji, lakini pia klabu za daraja la tatu nchini Ubelgiji na Ujerumani nazo pia zinamhitaji." alisema meneja huyo.

Hii si mara ya kwanza kwa Yanga kumhitaji straika huyo kwani nusura imsajili katikati ya msimu wa Ligi Kuu uliopita alipokuwa akiichezea Mwadui FC, lakini hawakuafikiana na dau walilotangaziwa hatimaye KMC ikamsajili.

Hivi karibuni Ilamfya alizichachafya ngome za timu hizo mbili, alipofunga bao kwenye mechi ya kirafiki Uwanja wa Uhuru, KMC ikiisulubu Yanga mabao 3-0, pia akifunga bao la kufutia machozi kwenye mechi kati ya timu yake dhidi ya Simba Uwanja wa Mo Arena, Bunju jijini Dar es Salaam, KMC ikibugizwa mabao 3-1.

Katibu Mkuu wa KMC, Walter Harrison, amesema kuwa hawana tatizo na klabu yoyote kuja kumchukua mchezaji wao, iwe Ilamfya au yoyote yule, ili mradi tu taratibu zifuatwe.

"Sisi hatuna tatizo na hilo, timu kama inamtaka waje tuelewane kwa sababu wachezaji wetu wana mikataba bado, tutakachokipata tutatafuta vijana wengine wenye uwezo wa kucheza soka ili na wao wajiuze. Hili ndilo soka, wengine watatoka na wengine wataingia," alisema.

## Mtibwa Sugar yaifuata kibabe Coastal

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa timu ya Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila amesema wana imani kubwa ya kuondoka na pointi zote tatu kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union utakaopigwa Juni 20.

Akizungumza na Nipashe, Katwila alisema kwamba, wamekwenda kusaka pointi tatu katika mchezo huo, hivyo wamejipanga kwa umakini mkubwa.

**"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata pointi tatu ugenini, li cha ya kwamba tunakwenda kucheza na moja ya timu bora kabisa kwe nye Ligi Kuu Tanzania bara," alisema Katwila.**

Kocha huyo alisema aliondoka jana na kikosi cha wachezaji 20 tayari kuwakabili Wagosi wa Kaya hao, mchezo utakaopigwa uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Aidha alisema kwamba, amebaini upungufu kadhaa katika mechi za kirafiki walizocheza na ameyafanyia kazi ili wasifanye vibaya kwenye mchezo huo.

## Nyota watatu Azam kuikosa Yanga

**Na Saada Akida**

WACHEZAJI watatu nyota wa Azam FC watakosekana kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Yanga utakaopigwa Jumapili hii kwenye uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Kocha msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, ameliambia gazeti hili kwamba, maandalizi kuelekea mchezo huo yanaendelea vizuri, lakini wachezaji Salum Abubakari 'Sure boy', Frank Domayo na Agrey Morris wataukosa mchezo huo.

Alisema Sure boy anaendelea na matibabu, huku Domayo anatumikia adhabu ya kadi 3 za njano pamoja na Morris bado hajawa fiti.

Alisema Morris alijiunga juzi na wenzake, Bruce Kangwa, Never Tigere na Nicholas Wadada kufanya mazoezi ya kujiweka fiti sababu ya kuchelewa kujiunga kikosini.


"Hivyo wachezaji hao pamoja na wale waliokwama Ghana kwa sababu ya "Lockdown", wanaweza kuukosa mchezo huo," alisema kocha huyo.

Aliwataja nyota hao waliokwama na Lockdown ni Yakubu Mohammed, Daniel Amoah na Razack Abarola ambaye ni kipa namba moja katika kikosi hicho.

# Michezo

Ijumaa Juni 19, 2020

Nipashe

**Barcelona yajiandaa kumpa Messi mkataba mpya**

HABARI UK 22



Kocha wa Riadha, Iddi Muhunzi, akitoa maelekezo kwa wanariadha wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati walipokuwa wanafanya mazoezi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, jana, kujiandaa na mashindano ya kitaifa yatakayofanyia Agosti jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## SVEN AZITAJA MECHI ZA UBINGWA

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kesho wakitarajia kushuka uwanjani kuumana na Mwadui ukiwa ni mchezo wao wa pili, tangu serikali kuruhusu michezo kuendelea kufuatia mlipuko wa virusi vya corona, Simba imeweka wazi michezo minne itakayowahakikishia ubingwa msimu huu.

Kocha wa vinara hao wa ligi, Sven Vanderbroeck amesema kuwa anaamini kama watachanga vizuri karata zao mechi kwa hizo nne zinazofuata zitatosha kuwahakikishia ubingwa.

Baada ya mchezo wa kesho dhidi ya Mwadui, Simba ina michezo miwili mkoani Mbeya dhidi ya Mbeya City na Tanzania Prisons kabla ya kuelekea Tanga kuumana na Coastal Union.

"Michezo mitatu ijayo ni muhimu sana kwetu, wachezaji wanafahamu hivyo na tumejipanga kuhakikisha kila kitu kinaenda sawa kama mipango yetu tulivyoipanga, ushindi katika michezo hii itatupunguzi kazi na presha kama mabingwa watetezi," alisema Sven.

Alisema kuwa anafurahishwa na namna wachezaji wanavyopambana na wanavyotaka kumaliza kazi mapema ya kutangazwa mabingwa watetezi.

"Lakini ni lazima tuwe makini katika kila mchezo, hatutawadharau wapinzani wetu kwa sababu tu tunaongoza ligi, tunafahamu kama tusipokuwa makini hatutatimiza mipango yetu," alisema.

Simba mpaka sasa wanaongoza ligi wakiwa na pointi 72 baada ya kucheza michezo 29, huku wakiwaacha kwa pointi 15 Azam FC wanaoshika nafasi ya pili na Yanga pointi 17 katika nafasi yao ya tatu huku timu zote zikiwa zimecheza michezo sawa.

# JKT YALALAMIKA YANGA KUBEBWA

## Kocha afunguka mwamuzi hakuitendea haki timu yake, Lamine amwomba radhi Kazimoto na TFF, Serikali yaifungia JKT kwa kujaza mashabiki...

**Somoe Ng'itu, DODOMA na Faustine Feliciane**

WAMEBEBWA! Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Abdallah Mohammed "Bares" amesema mwamuzi hakuitendea haki timu yake kwa kuruhusu mpira kuendelea na hatimaye Yanga kupata bao la kusawazisha wakati mchezaji wake akiwa amefanyiwa madhambi na nyota wa wapinzani wao.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi jijini hapa, Yanga ilikubali kulazimishwa sare ya bao 1-1, dhidi ya Maafande hao ambao sasa wamehamia kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Akizungumza na Nipashe jana, Bares alisema makosa ya mwamuzi ndiye yaliiumiza timu yake katika mchezo huo ambao wao walitangulia kupata bao kwenye kipindi cha kwanza kupitia kwa beki wake, Michael Aidani.

"Kwanza namshukuru mwamuzi maana pale alipochezesha ndio uwezo wake, ni binadamu anaweza kukosea, lakini hii ilikuwa wazi kwamba mchezaji wangu alifanyiwa faulo kwanza na yeye aliendelea kuchezesha," alisema Bares.

Aliongeza kuwa hamlaumu golikipa wake, Abdulrahman Mohammed kwa kitando cha kutema mpira jirani na mshambuliaji wa Yanga na kueleza hilo ni tukio la kawaida katika mchezo na mlinda mlango huyo amewasaidia kupata matokeo mazuri katika michezo mbalimbali iliyopita.

Kocha huyo alilalamika kiungo wake, Mwinyi Kazimoto aliyepigwa teke na beki wa Yanga, Lamine Moro kuonyeshwa kadi nyekundu wakati hakufanya kosa kutokana na wachezaji wengine kufanikiwa kumdhibiti ili asirudishe shambulio hilo.

"Mwinyi Kazimoto amepigana wakati gani? Wakati wachezaji wa Yanga walikuwa wanapambana kumshika asipigane, hata sisi makocha tuliingia kumzuia na tulitaka kumtoa, ila hata mimi nimewalaumu wachezaji wangu kwa kuonyesha hamaki, hawakutakiwa kufanya hivyo, walipaswa kukubaliana na mwamuzi kwa sababu yeye ni sehemu ya tatu ya mchezo, mwamuzi wa kati hakuwa makini, hakuliona tukio wakati yeye alikuwa karibu na mchezo," Bares alisema.

### LAMINE AOMBA RADHI

Beki wa Kimataifa wa Yanga kutoka Ghana, Moro ameomba radhi kwa Watanzania, wachezaji wenzake, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kitendo chake akichofanya cha kumpiga teke Kazimoto.

Lamine pamoja na Kazimoto ambao walitolewa nje kwa kadi nyekundu, amesema tukio hilo halikuwa la kiungwana na anajutia kwa kufanya hivyo.

Beki huyo alisema pia amempigia simu kiungo huyo wa zamani wa Simba, Kazimoto kumwomba radhi kutokana na kosa alilofanya.

Hata hivyo, taarifa kutoka Yanga zilieleza Moro atakatwa faini ya Sh. milioni moja katika mshahara wake kutokana na kitendo hicho kama kanuni na taratibu za klabu yake zinavyosema.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema klabu yao haikufurahishwa na kitendo hicho na inawaomba radhi wadau wote wa soka akiwamo Kazimoto.

Bumbuli alisema kikosi cha Yanga kilirejea jijini Dar es Salaam jana na jioni kilitarajia kuanza mazoezi kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Azam FC utakaochezwa Jumapili usiku kwenye Uwanja wa Taifa.

Wakati huo huo, serikali imetangaza kuiadhibu klabu ya JKT kwa kitendo cha kuruhusu mashabiki wengi uwanjani katika mchezo wa juzi dhidi ya Yanga, ambapo walikaa kwenye majukwaa bila kufuata maelekezo yaliyotolewa ya kujikinga na ugonjwa wa mlipuko wa virusi vya corona.

Katika taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo iliyotolewa jana, imeeleza kuwa sasa JKT itacheza michezo yake yote kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Jamhuri jijini Dodoma bila mashabiki.

Taarifa hiyo imefafanua kuwa katika mchezo huo namba 288, JKT walikiuka kanuni 2.0.2(iii) inayosisitiza watu kuachiana mita moja.

"Hatua hii inalenga kuvikumbusha vilabu wenyeji, wasimamizi na wadau wa michezo kuendelea kusimamia muongozo wa afya na taratibu nyingine michezoni hadi hapo serikali itakapojiridhisha kuwa ugonjwa wa Covid-19 umekwisha kabisa hapa nchini, na hatua hizi zinalenga kuwalinda wananchi, wachezaji wenyewe, viongozi na Watanzania kwa ujumla," ilisema sehemu ya taarifa hiyo iliyosainiwa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Lorietha Lawrence.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002